Mambo ambayo yanahusu energy, kama ni katika nyumbani kama ni katika viwandani na mahali pengine, lazima itafutwe njia ambayo haidhuru mazingira na ninaunga mkono Prof. Wangari Mathai katika kupigania mazingira. Maneno yake yapate kusikilizwa kwa sababu yatatusaidia sisi, sio yake peke yake. Yeye pia ni mwananchi wa Kenya asikilizwe na maneno yake yasikilizwe na kuzingatiwa.

Na resources vile ambazo ni vigumu hawezi ku-replace kama mafuta, kama vitu vingine ambavyo huwezi ku-replace, lazima itumiwe kwa kiwango kidogo kwa njia ambayo inafaidi watu wote. Ingingine ni kwamba preserve i-replaceable resources. Na kama ardhi ni kitu ambayo haizai, sasa baba kama ako na acre ishirini akitugawanyia, halafu mimi nikuje kumgawanyia mtoto wangu halafu mtoto wangu atagawanya, tutagawa mpaka wapi na haizai. So itunzwe jinsi ilivyo.

Na jambo la mwisho, ni kwamba sharti population clause ikuwe controlled katika hali yoyote ile. Kama ni watu ambao ni citizens basi wazae katika njia ambayo wanaweza kujitunza wenyewe, ili watu wasizae na kuwaachia watoto watu wengine kuwatunza. Mimi sitaki kubebeshwa mzigo ya mtu mwingine. Nataka mimi nijitahidi katika hali yangu, nifanye kazi yangu nitosheleze nyumba yangu, lakini nisibebe ya mwingine. Kama ni mambo ambao yanatokea katika hali ya kiulimwengu, basi tusaidiane tusaidie wasiojaaliwa. Na hiyo kama ni family planning ifanyiwe na ifundishwe tena zaidi, katika kila mahali katika nchi hii.

Na ninayo mambo yanahusu immigration: Immigration watu ambao wanahamia nchi hii wazuiliwe kwa sababu wasikuje kuwacha mizozo katika nchi yao na kuja kutuletea mizozo ama kuja kutufinya kwa jinsi ambavyo tunaishi sisi. Serikali itunze hiyo ili tupate kuendelea vizuri katika kujenga taifa letu na kuitunza.

Com. Lenaola: Jambo la mwisho.

Pastor Sammy Lagat: Jambo la mwisho, nikuhusu transfer of power. Kama Rais amechaguliwa, achaguliwe kwa wakati fulani na akae mpaka muda fulani ili achukue madaraka. Na madaraka hiyo lazima ifanywe kwa njia ya heshima, kwa yule ambaye anakuja madarakani na mwenye anaondoka. Hata kama alishindwa vibaya lakini akubali kupeana hiyo madaraka kwa njia nzuri, sio kama vile mambo inafanyika Madagascar. So tuwe na hali ya heshima katika nchi yetu. Tuitunze nchi yetu, tuiendeleze nchi yetu ili tufikie katika ukuaji wa viwanda ifikapo mwaka wa elfu mbili na kumi na tano. Asante sana.

Com. Lenaola: Asante sana Pastor. Uko na memorandum zingine, hizi nizako ama?

Pastor Sammy Lagat: Ninapeana.

Com. Lenaola: Lakini niko na swali. Unajua ulisema kwamba tutoe polygamy unajua kwamba kuna pia heshima kuabudu katika nchi, pia ungependa hiyo ikuweko si ndio? Na nitamaliza swali. Na Waisilamu wanakubaliwa kuoa wanawake wane.

Si wakatazwe pia kuoa kwa sababu mila yao inakubali?

Pastor Sammy Lagat: Ninasema ya kwamba sheria moja iwe katika nchi hii, sio hali ya dini hii na dini hii. Kwa sababu polygamism is violation against human rights. Hata kama niya Kiislamu. Nataka nchi hii itauliwe na sheria moja hata ile inaitwa Chief Kadhi court hiyo iondolewe na hii nchi iwe na court moja. Kama kanisa langu itapewa ikuwe na court yake, na mambo hayo yote na mahakama yake, na hayo mambo mengine, dini hii inakubaliwa kuwa na polygamism na dini hii haikubaliwi inaleta hali ya taarugi katika nchi hii. Nataka tuwe na sheria moja na utawala ambao unaruhusu watu wote kuishi vizuri bila kubagua watu tofauti tofauti ama watu wa dini tofauti tofauti.

Com. Lenaola: Asante sana Pastor. Basi jilandikishe pale na upeane memorandum. Joseph Kalasinga. Wapi Kalasinga? Lumuai Nicholas. Wewe endelea.

Nicholas Lumuai: Jina langu naitwa Nicholas Lumuai. *Soroh nyoma ompo katiba 'nn ketu wol.*

Translator: Anasema kwamba ni pongezi kwa watu wa Katiba ambao wamefika hapa.

Nicholas Lumuai: *Mi kugh nyo kesusecha wol.*

Translator: Anasema kuna jambo moja ambalo limetusumbua sana watu wa upande huu.

Nicholas Lumuai: *Nyo ngwan ompo wanainchi.*

Translator: Anasema ni uchungu sana kwa wananchi.

Nicholas Lumuai: *Ato igh chi makosa.*

Translator: Anasema mtu akikosa.

Nicholas Lumuai: *Mi pchai klentoy AP.*

Translator: Kuna watu ambao wanaitwa Administration Police.

Nicholas Lumuai: *Ato nyoru chii*

Translator: Hawa watu wakipata mtu ambaye anapenda kosa.

Nicholas Lumuai: *K'tomoh kesuwa loh kegh makosa.*

Translator: Kabla mtu huyo hajaonekana kwamba alitenda kosa.

Nicholas Lumuai: *Ketugh nyopoh nyoman.*

Translator: Hawa watu huwa wanamshika na kumchapa.

Nicholas Lumuai: *Pchoni katugh ng'oru cho sopchot.*

Translator: Anasema hawa watu wanachapa watu kiasi kwamba wengi wanaaga dunia na wachache ndio wanaweza kupona.

Nicholas Lumuai: *Omokan loh*

Translator: Basi anapendekeza kwamba.

Nicholas Lumuai: *Ato igh chi makosa*

Translator: Mtu akitenda kosa.

Nicholas Lumuai: *Kep mpaka Court*

Translator: Anapendekeza kwamba mtu huyo hawezi kupelekwa hadi kortini.

Nicholas Lumuai: *Ato kanam makosa.*

Translator: Akipatwa kwamba yeye ndiye amekosa.

Nicholas Lumuai: *Kerat*

Translator: Basi korti iamue jinsi ambavyo wataweza kumfanyia.

Nicholas Lumuai: *Moh karam nye keswang chii.*

Translator: Anapendekeza kwamba mtu yeyote asichapwe ama asizurutishwe kwa vyovyote.

Nicholas Lumuai: *Nyopoh odeny,*

Translator: Jambo la pili.

Nicholas Lumuai: *Atomimchango korr nyo kakipitishan.*

Translator: Kukiwa na mchango katika sehemu fulani ambayo imepitishwa.

Nicholas Lumuai: *Mokino wazazin kukonu letino chomoy onto wono kikeghanta.*

Translator: Anapendekeza kwamba ni heri wazazi waweze kutoa vile ambavyo imependekezwa.

Nicholas Lumuai: *Wolo mohmokonye kirwokot kpesteah kori pich ogh'o.*

Translator: Anatoa hoja kwamba chiefs wasitembee katika nyumba za watu usiku eti wanatafuta michango.

Nicholas Lumuai: *Tukul kowow chaa pestoo ogh'o.*

Translator: Anasema kwamba si binadamu ndiye anaweza kufua nyumba ya watu tu, bali ni mnyama wa mtu, mfano ya fisi.

Nicholas Lumuai: *Nyopoh somok.*

Translator: Jambo la tatu, anapendekeza kwamba chiefs waweze kupigiwa kura ama mlolongo.

Nicholas Lumuai: *Moroy kirwokot kepur kura.*

Translator: Inatakikana chiefs wawe wa kuchaguliwa na raia.

Nicholas Lumuai: Ato igh makosa.

Translator: Ili akitenda jambo fulani ambalo ni mbaya ama kosa.

Nicholas Lumuai: *Ku acha cho kifutonoy.*

Translator: Basi ni sisi wenyewe ndio tunaamua kumfuta.

Nicholas Lumuai: *Wolo ato kito application*

Translator: Lakini nikisema kwamba hawa wana-apply.

Nicholas Lumuai: *ng'uno chii ata koroo Turkana, akuluku chief.*

Translator: Watu ambao wanatoa mahojiano mtu anaweza kutoka sehemu za Turkana ama sehemu zingine na akuje akuwe chief wa sehemu zingine.

Nicholas Lumuai: *Moghomoy nye kirwokin k'swang' chii.*

Translator: Anasema kwamba chief sasa hawezi kutungwa mlolongo na asikuwa na sheria yoyote ya kuweza kuguza mtu yeyote.

Nicholas Lumuai: *Nyo poh angwan.*

Translator: Jambo la nne.

Nicholas Lumuai: *Mi poltinoh cho mi woletee.*

Translator: Kuna shamba vidogo vidogo plots.

Nicholas Lumuai: *Chay poh center.*

Translator: Ile imetengwa katika soko.

Nicholas Lumuai: *Moghomoy nye kegh application.*

Translator: Anasema kwamba haifai kuwa applied.

Nicholas Lumuai: *Ompo wolo ato kiapplayn nyoru pich cho lowoch k'lyo pchini poh koronini.*

Translator: Ikiwa tutaruhusiwa kutuma maombi kwa watu fulani, watu hawa hawawezi kujua nani anatoka wapi. Na watapata plots na wenyeji wakose.

Nicholas Lumuai: *Omokan kutotoh wazee chopoh koronini.*

Translator: Wazee wa area wawe wakipeana plots

Translator: Basi yake ni hayo.

Com. Yano: Asante sana. Kalasinga Loshek. Endelea.

Kalasinga Loshek: Mimi naitwa Loshek Kalasinga. Mimi natoka Nakwijit.

Translator: Basi anasema anatoka sehemu inaitwa Naguchit.

Kalasinga Loshek: *Soroh ompo katiba 'n poh asete.*

Translator: Anasema shukurani sana watu wa Katiba ama Katiba ya leo.

Kalasinga Loshek: *Ompo wolo kimii nyo kipoh kohny, nyo kimoh kswechanye.*

Translator: Anasema kulikuwa na katiba ya awali ambayo hata sisi hatujui.

Kalasinga Loshek: *Akitung 'o cha konyin amakuswechanye.*

Translator: Anasema ni Katiba ambayo ilituzuia macho na hatukuiskia au kuona, hatujui vile ilikuwa.

Kalasinga Loshek: *Mominye school korenyan.*

Translator: Anasema sehemu yake ya Naguchit hakuna shule.

Kalasinga Loshek: *Mii ng'olyon akong' nyo omwoghan.*

Translator: Anasema kuna jambo lingine.

Kalasinga Loshek: *Mii chi nyo ko kengsho*

Com. Yano: Apendekeze shule kwanza.

Kalasinga Loshek: *Omoran ketek school koronona.*

Translator: Sasa anapendekeza kwamba serikali waweze kujenga shule sehemu hiyo.

Kalasinga Loshek: *Mominye tukul koronona parapara.*

Translator: Na anapendekeza pia jambo la barabara. Kwamba anasema sheria haina barabara.

Kalasinga Loshek: *Mokecha ketek school.*

Translator: Na anataka shule zijengwe.

Kalasinga Loshek: *Ketek nyole kitee, atoni.*

Translator: Anataka shule zijengwe sehemu hiyo, ili watoto wapate mahali pa kusomea.

Kalasinga Loshek: *Ompo wolo kipohlecha.*

Translator: Anasema sisi tumeshindwa.

Kalasinga Loshek: *Kakiyltecha monung'ee paat .*

Translator: Sasa ile kazi imebaki kwao sasa nikupeana wasichana waoleke tu kwa sababu hakuna shule sehemu hiyo.

Kalasinga Loshek: *Keyiltecha monung'ato mominye school, atolapai, kerupacha asl toh nyo.*

Translator: Sasa anasema kwamba kama shule hakuna basi tunapeana watoto wetu kuolewa na sisi tunakaa na ile mila yetu ambayo ilikuwa pale.

Kalasinga Loshek: *Yilto pich cho chang' monung', melo chi akong'a.*

Translator: Ana amini kwamba huyo mtoto ambaye anaoleka huwa mtu mmoja hapeani ni watu wengi.

Kalasinga Loshek: *Papoto monung' nko papoto karchnin.*

Translator: Baba ya huyo msichana na baba ya yule ambaye anamuoa.

Kalasinga Loshek: *Chitukul nko yoo nyi.*

Translator: Pia akina mama wote wa pande yote mbili.

Kalasinga Loshek: *Ah kakip yee nyu keng'un chi kau.*

Translator: Sas mtu anakuja halafu anaoa mke wake.

Kalasinga Loshek: *Kerat nyo klentoy trum.*

Translator: Na huyo msichana atapewa pete.

Kalasinga Loshek: *Nko t'kole karrn.*

Translator: Pete niya aina ya ngozi. Anasema pete kwa sababu ni aina ya ngozi ambayo inawekwa kwa mkono.

Kalasinga Loshek: *K'loh anka nyo poh odeny.*

Translator: Ya pili, anasema kuna hawa watu wa kanisa.

Kalasinga Loshek: *Miteni pchai poh kanisa.*

Kalasinga Loshek: Ngu'noy chi koyogh toh nyi.

Translator: Mtu anakuja kwako kukuletea posa ama hutaki kuoa msichana kwako.

Kalasinga Loshek: *Kwip kameto montanyi*

Translator: Anaoa mke wake.

Kalasinga Loshek: *Ng'unoy nko kame nko paponyi.*

Translator: Na baba yake na mama yake ndio watapeana.

Kalasinga Loshek: *Totoh pipo kanisa trum akong'a yeu.*

Translator: Anasema hawa watu sasa huwa wanapeana pete moja tu kwa mkono pale.

Kalasinga Loshek: *Ompo wolo poru lo.*

Translator: Hii inaonyesha ya kwamba.

Kalasinga Loshek: *Kokonu poh chi.*

Translator: Hiyo pete inaonyesha kwamba huyo ni mke wa mtu.

Kalasinga Loshek: *Ompo wolo moting' nyee tip'n trum.*

Translator: Kwa kuwa wasichana hawatakuwa na pete yeyote.

Kalasinga Loshek: *Nyara muma Pokoot nyo mowetonye tohkunyoru nyo poh chii.*

Translator: Anasema sasa ni jitihadi kubwa kwa wa Pokot kwamba yule ambaye ana hiyo pete ama hiyo ngozi kwa mkono ni mke wa mtu na hatafikani afukuzwe.

Kalasinga Loshek: *Ng'olyonto Pokoot nyoni nyo kipoh Kohny.*

Translator: Anasema hiyo ndio ilikuwa mila yw wa Pokot ya zamani.

Com. Yano: Pendekezo.

Translator: *Imorenyi kegh lohnee?*

Kalasinga Loshek: *Topoo lenyoni ng'ala trum toh kuwagh chii kipo chii.*

Translator: Anasema sasa hiyo ibaki hivyo hivyo ili watu wengine hawawezi kukutambua kwamba huyu ni mke wa mtu.

Kalasinga Loshek: *Atorapas karchnin.*

Translator: Anasema mwingine anaweza oa halafu mume anaweza aga dunia.

Kalasinga Loshek: *Chichona kikwal parenyi,*

Translator: Na huenda huyo kijana ambaye ameaga dunia alikuwa amenunua shamba lake.

Kalasinga Loshek: *Kloh korketo, ocheng'an paranu kwegh katanchara.*

Translator: Sasa huyu mke anaweza geuka kwamba shamba hili sasa liende kwao – kwa baba yake.

Kalasinga Loshek: *Ompo achaa Pokoot.*

Translator: Kwa sisi Pokot sasa.

Kalasinga Loshek: *Papoto Wero korapas nyo paito pare ngo monung'.*

Translator: Desturi yetu kama wa Pokot ni kwamba yule kijana ambaye aliaga dunia baba yake ndiye anahitaji kuchunga mali hiyo yote pamoja na huyo mke ambaye ameachwa na mumeo.

Kalasinga Loshek: *Krkegh kotoghoy kama monung' katah, topoh otin, akung'unoy chitonyi katah.*

Translator: Anasema kwamba hata kama huyu mke vile alifiwa na mumeo anakataa hapa nyumbani, inafaa akae hapo mpaka akipata mume mwingine ambaye anatoka mbali huyo mume ambayo amefuata anatakikana atoke kule aje huku.

Kalasinga Loshek: *Aku pontonete poh kayete nyo totoy.*

Translator: Na huyu baba wa hii familia ndiye ana mamlaka kwa huyu mke ya kumpeana tena.

Kalasinga Loshek: *Nko werkachii.*

Translator: Na vijana wake wavulana wakubwa.

Kalasinga Loshek: *Ngo'lyon anka.*

Translator: Jambo lingine.

Kalasinga Loshek: *Mii monechara cho ipunoh kameto montanyi wolo low.*

Translator: Kuna watu ambao wameweza kufanya kazi na wanaweza kuja na wake zao kutoka mbali.

Kalasinga Loshek: *Ngu,noi chichonoh ngo kametomontanyi nyo puratee.*

Translator: Akiingia huku anakuja na mke wake ambaye amemvalisha vizuri.

Kalasinga Loshek: *Wolo otino ngu'noy, koh madam?*

Translator: Huenda ikawa huu mke ni madam.

Kalasinga Loshek: *Kungu'n nko nga'lechi chopo koreng'waa.*

Translator: Sasa anasema kwamba huyu mke ametolewa mbali na anakuja kutuletea mila ya huko kwao.

Kalasinga Loshek: *Kungu'n nko s'ra nyo tenoh.*

Translator: Anakuja na mini skirt, nguo ambayo ni fupi sana.

Kalasinga Loshek: *Nyini kotopoloh, kut yomat.*

Translator: Anasema ni jambo la aibu sana kwa sababu akikaa chini kidogo hivi na nguo inaweza inuka.

Kalasinga Loshek: *Kloh acheng' kigh nyomi yum kuwo s'ra kutoch.*

Translator: Anasema kwamba akitaka kutoa kitu ambayo iko juu kidogo basi ile nguo inainuka.

Kalasinga Loshek: *Achaa Pokot,ktoghechaa ng'alechona.*

Translator: Anasema sisi kama wa Pokot tunakana jambo hili kabisa.

Kalasinga Loshek: *Kamokecha k'mi s'ra yii (he demonstrates)*

Translator: Anataka akina mama wavae nguo ambayo inafika chini ya magoti kabisa.

Kalasinga Loshek: *Mii ng'olyon anga yara*

Translator: Basi kuna jambo lingine hapa.

Kalasinga Loshek: *Kungun chichai napo nko kokonyontenyi yii.*

Translator: Bado anaongea juu ya wale watu ambao wametolewa mbali.

Translator: Anasema mtu anaweza kuja na mke wake.

Kalasinga Loshek: *Antoh nyini leh madam ongut.*

Translator: Ama huyo ambaye ni madam tu.

Kalasinga Loshek: *Atowestoo nko Pokoot.*

Translator: Anasema akiwa anatembea tembea na wa Pokot.

Kalasinga Loshek: *Kuchengu' koti nyolenye nyu*

Translator: Analeta koti kama hii.

Kalasinga Loshek: *Nko shati nyolenye nyara.*

Translator: Na sharti kama hili lake.

Kalasinga Loshek: *Nko long.*

Translator: Halafu ya mwisho analeta suruali ndefu.

Kalasinga Loshek: *Acha pokoot m'kchomechanye ng'ale chu.*

Translator: Pia sisi wa Pokot hatupendelei sana mavazi kama hayo.

Kalasinga Loshek: *Kalukunee s'ra nu toh kulak kama monung' akopoh poy.*

Translator: Anasema kwamba ni nini imefanya hii long itolewe kwa wazee mpaka akina mama.

Com. Lenaola: Pendekeza.

Kalasinga Loshek: *Mokino kwit s'ra yoo kutugh , akurat lenyaye poh Kohny.*

Translator: Anasema kwamba akina mama kuna nguo zao ambazo zinajulikana. Wavae rinda na wanaume wavae long.

Com. Lenaola: Haya jambo la mwisho.

Kalasinga Loshek: *Korenchaa nyopoh pokoot, mokecha k'mii pokotu opun, atachosomoni, tohkumwowechara ng'al.*

Translator: Anasema kwamba huwa tuna shida kama wazee. Tukienda sehemu zetu kama Kapenguria ambayo ni Headquarters yetu, huwa tunapata watu mbali mbali. Hata communication ni shida. Tungependelea kwamba watu wenye watakuwa pale wawe ni wa Pokot wenyewe ili tuweze kuwasiliana nao vizuri.

Kalasinga Loshek: *Kiolan yara kot nyo iruwoi ompo kapenguria, kelenachnun: naka.*

Translator: Basi huwa akienda kule huwa anapata shida sana akitaka kazi, akitaka mahali pa kulala huwa wanaambiwa tu toka.

Kalasinga Loshek: *Onto kosomoy pough!*

Translator: Ama akitaka kuomba maji.

Kalasinga Loshek: *Kelo, ngu'no ono nyara t'ng'etoo sarangwach.*

Translator: Wanasema mtu huyo ambaye ana mavazi aina hii anatoka wapi?

Kalasinga Loshek: *Komokan k'mii nyole pochon, toh ku'ngut loh kalenye nyoni poyii choani kung'ata otini leh kohny.*

Translator: Sasa anapendekeza kwamba sehemu ya mtu iwe ni ya mtu, ili mzee akienda yule kijana wake m-Pokot ambaye

yuko pale anamuelewa kwamba baba yangu ama wazazi wetu wanafanana hivi.

Kalasinga Loshek: *Kokarchan atoni.*

Translator: Anasema mambo yangu yamefika pale.

Com. Lenaola: Asante sana Bwana Kalasinga. Jindikishe pale. Paulo Lungolian. Halafu wale ambao niliwaita asubuhi na wamekuja sasa, nitawaita baada ya kumalizana na wengine. Kwa hivyo mtulie tu kawaida hiyo list ya kwanza.

Paulo Long'eleya: *kurenann Paulo Long'eleya*

Translator: Jina lake ni Paulo Lung'elian

Paulo Lung'elian: *Soroh nyoman Ompo nnga'la katiba.*

Translator: Anasema ni asante nyinyi watu wa Katiba ambao mmefika hapa ili tuweze kuwasiliana nanyi.

Paulo Lung'elian: *K'mwoghechaa ng'ale chini kipo kohny.*

Translator: Anasema sisi tulisema mambo ambayo ilikuwa ni ya desturi yetu.

Paulo Lung'elian: *Mii chii nyo yiyoy tip'n cho chang'. Ato yilta nyoru tich cho chang' akuluku chichai s'kon.*

Translator: Anasema kwamba hapo zamani mtu akiweza kuzaa watoto wake wasichana wengi, huwa kuna tunaweza kupata mali kutokana na hawo wasichana – unaweza kuwa tajiri.

Paulo Lung'elian: *Kiyiltonecha monecho, leh otini kipo Kohny.*

Translator: Sasa anapendekeza kwamba wazee wa upande wote mbili, yule msichana ambaye anaolewa na yule kijana ambaye anaoa huwa wanazungumzia wale ambao wanaoana kwa njia nzuri na angependa hiyo hali ibaki hivyo.

Paulo Lung'elian: *Omokan sokoni tich kepu Kapenguria to kuwetu faida nyo rumu ompo tich cho kioltoy. Chang' ropiyeen cho wonyegho arawet.*

Translator: Basi anaongea kama mkulima kwamba yeye ni mkulima wa ng'ombe na huwa anapata shida kubwa sana ya soko. Huwa anapeleka ng'ombe kutoka sehemu yake ya Kacheliba na anapeleka huko Nairobi sehemu ambayo inaitwa

Dagoretti. Na kwa njia huwa anatomia transport nyingi sana mpaka hana faida yoyote. Sasa anapendekeza kwamba soko kubwa iweze kutengwa hapa Kapenguria ili aweze kupata faida kutokana na mifugo yake.

Paulo Lung'elian: *Tokegh maendeleo, makino ktossu chi ng'olyon. Mokpshininye chi akong'a.*

Translator: Anasema kwamba kwa ukweli hapo awali ni wazi kwamba mtu hawezi kuweza kufanya sehemu yake iendelee ila anawezaungana na wenzake wabadilishana mawazo ili sehemu yao iendelee.

Paulo Lung'elian: *Keleta tagh ompo choni. Kiowan nko Bumala, Mwoghoy chipoh mtkaa loh faida tany ku miasaba, mianane. Roko kegh makt poh tich yii le Kapenguria.*

Translator: Sasa anarudia hoja yake ya kwanza kwamba huwa anapeleka ng'ombe huko Dagoretti, Bumala lakini ile faida anapata anaweza pata shilingi mia nane kama ni zaidi na akirudi nyumbani huwa anapata pesa hizo zimeisha. Basi anarudia kwamba soko kubwa iweze kuwekwa hapa Kapenguria.

Paulo Lung'elian: *Tenoh choni chichan.*

Translator: Hiyo tu.

Com. Lenaola: Jiandikishe. Joseph Lokomol.

Joseph Lokomol: *Kurenann Joseph Lokomol*

Translator: Jina lake ni Joseph Lokomol.

Joseph Lokomol: *Location toh nyan yii le Sook.*

Translator: Yeye anatoka location ya Sook.

Joseph Lokomol: *Ng'olyontenyany nyo tagh..Omwoghan loh kanyakusoman monung'o Kenya k'le ng'ata kopoh akon'ga mpaka university.*

Translator: Jambo lake la kwanza. Anapendekeza kwamba elimu ikuwe niya bure kuanzia darasa la kwanza hadi kiwango cha chuo kikuu.

Joseph Lokomol: *Ong'ololenan ng'ala nyung'utian.*

Translator: Pia yeye anaongea juu ya udongo.

Joseph Lokomol: *Mi ng'ala cho mi katibanai poh turu.*

Translator: Anasema katika Katiba ya kwanza ambayo ilikuwa ni ya giza.

Joseph Lokomol: *Kimwoghoy loh ghamoy chi nyungutian ngo serikali, atorumu kigh mpo nyungutiandanini kupar kwen nko serikali le turkwell.*

Translator: Basi huyu anapendekeza kwamba kwa hali ya udongo anapendekeza kwamba mali ambayo itapatikana kwa ile shamba ya mtu iweze kugawanwa katikati serikali nusu na mwenye shamba nusu.

Joseph Lokomol: *Lenye ma yai poh Kasitei.*

Translator: Anaongea juu ya nguvu ya umeme ambayo iko kwa Turkwell.

Joseph Lokomol: *K'mwoghecha loh.*

Translator: Anasema kwamba.

Joseph Lokomol: *Pokot chi mi kiono korejnjaa.*

Translator: Anasema sisi kama Pokot sasa ambao sehemu hiyo ama mahali iko katika shamba letu ama kwetu.

Joseph Lokomol: *Mokechaa kechagh kiona kwen, chichi nusu poh serikali nusu.*

Translator: Anataka yote ambayo yanatokana na moto huo igwe katikati nusu iwe ya Pokot nusu iwe ya serikali.

Joseph Lokomol: *Pich cho mong'oi koroo nino kikrohss nyinoh kicheng nanam.*

Translator: Wale ambao walikuwa wanaishi mahali ambapo palitengwa kwa ajili ya maji hayo.

Joseph Lokomol: *Mokino k'yar serikali woloh mong'oi pchono kimii wolonii.*

Translator: Anasema kwamba utapata kwamba mahali hapo watu walikuwa naishi na vile serikali walitenga kwa ajili ya maji, hawa watu wakabaki bila shamba. Sasa anauliza kwamba serikali waweze kutafuta shamba ama jinsi ya kuweza kupatia hawa wapate kuishi kama walivyo hapo awali.

Joseph Lokomol: *Akuross pchoni puchu poh KenGen mii yii poroh ktek schooltin cho mii koronini k'le, akusomeshan monee chinii free.*

Translator: Anasema kwamba wale wa KENGEN waweze kujenga shule pale bure na pia masomo iwe niya bure kutokana na ile pesa inatokana na hiyo nguvu ya umeme.

Joseph Lokomol: *Ngo skatal, ombo wolo ato chang'it pough kuwagh pich rumpoh.*

Translator: Basi anapendekeza hata hawa watu pia waweze kujenga hospitali ili iwasaidie wale watu kwa kuwa maji haya yaleta mbu ambayo pia inaleta ugonjwa wa malaria.

Joseph Lokomol: *Ngo'lolenan paitagh yee nyu.*

Translator: Basi anataka kuongea juu ya uongozi.

Joseph Lokomol: *Mokinoh kirwokin ketopoy ak'chi nyole konyis chokikwit tamanut somok.*

Translator: Ametaja kuwa anataka kuongea juu ya chiefs.

Joseph Lokomol: *Councillor; mokino nyo mukoi kusoman aku kirroy.*

Translator: Anapendekeza kwamba chief anatakikana awe mtu ambaye amekomaa, mtu ambaye amehitimu miaka thelathini na pia aweze kudungwa mlolongo ama kupigiwa kura. Basi anapendekeza kama yule mzee wa kwanza kwamba Councillor awe mtu ambaye anaweza kuandika na kusoma. Lakini kiwango cha elimu haijalishi

Joseph Lokomol: *Mokino kuross serikali wolo stutoh Sombrr nko Pokot ompo masomo ombo wolo kropu' pch' poh kyak.*

Translator: Basi anaongea juu ya jamii ambazo walikuwa disadvantaged wapewe affirmative action ili waweze kuletwa juu kimasomo kulingana na wengine.

Joseph Lokomol: *Omwowan nga'la tip'n cha k'mutoy.*

Translator: Pia anataka kuongea juu ya wasichana ambao wanapaswa tohara.

Joseph Lokomol: *acha pokot*

Translator: Sisi kama Pokot.

Joseph Lokomol: *Mokecha ketagh ompowolo kenyar masomo monung'*

Translator: Pia yeye amekubali kwamba kutairi kwa wasichana kupigwe marufuku. Kwa sababu kutairiwa kumezuia sana elimu

Joseph Lokomol: *Tok'mut monung' nyole chptoh ,kwich kegh loh kalukwan korka.*

Translator: Basi kwa sisi kama wa Pokot msichana akitairiwa hiyo ni kuonyesha kwamba msichana huo juu tayari kuoleka wakati wowote.

Joseph Lokomol: *Akaparta kumpo yiyoh, kataghan ng'ale chona.*

Translator: Basi anasema kwamba hiyo tumepiga marufuku.

Joseph Lokomol: *On'gololenan monung' nyo mi katangwa*

Translator: Pia anaongea juu ya msichana akiwa kwao.

Joseph Lokomol: *tomi monung' nyo le tyo akmi werkokwaa ombo kong'waa.*

Translator: Anaongea kwamba msichana akiwa kwao kuna wale mandugu zake wa kiume ambao wako pale.

Joseph Lokomol: *Mokitoninye par ontosh tich ompo kyiini.*

Translator: Anasema kwamba yule msichana hana hafasi ya kupewa ng'ombe ama shamba pale.

Joseph Lokomol: *Woloo tomiteno kokonyonda nyo koyu monechi chole tip'n lopai, k'muloy malik ko kong'waa.*

Translator: Anasema kwamba kunaweza kuwa na uwezekano kwamba mama fulani amepata tu wasichana katika nyumba yake. Basi ikiwa hakuna mvulana yeyote hiyo boma hawa wasichana wana nafasi ya kurithi mali yote ya boma hiyo.

Joseph Lokomol: *Yee nyu chii nyo katugh chii.*

Translator: Pia angependa kuongea juu ya mtu ambaye ameuu mwenzake.

Joseph Lokomol: *Ato mi chii nyo katugh chii.*

Translator: Ukiwa na mtu ambaye ameuu mtu.

Joseph Lokomol: *Mokino kegh lapai katangwaa ongut, meloh witooy kaporr.*

Translator: Kuna fine ambayo inaitwa “Lapai” ambayo anasema kwamba baba yule aliuu mtu wanahitajika kuchukua mali kwa mwenye aliuu sio kwamba iende kwa hata relatives.

Joseph Lokomol: *Akerat chichonoh konyiss tamanuut odeny. Ompo wolo susoy pchino atosuwiyii kuwestoo.*

Translator: Basi anapendekeza kwamba huyu mtu akipelekwa kortini inafaa afungwe miaka ishirini kwa kuwa akija kwa jamii tena inasumbua wale ambao walipoteza mtu wao kwamba huyu hai na wetu amepotea.

Com. Lenaola: Jambo la mwisho.

Joseph Lokomol: *Ng’ala sholut chopoh korr.*

Translator: Anasema kuna migogoro katika nchi ama kutosikizana.

Joseph Lokomol: *Ghomoy poyon nyopoh otini kuwang’ ng’alechona. Mominye ng’ala kotiki ompo kesi parr, kiwong’ o location.*

Translator: Anasema kwamba kukiwa na mzozano kati ya watu fulani ikiwa ni mambo ya shamba ama mambo mengine anapendekeza kwamba wazee watengwe wa kuweza kusuluhisha maneno hayo kwa hapo, bila kuendelea mpaka kortini.

Joseph Lokomol: *Akuliponoy serikali poyii chonii.*

Translator: Na hawa wazee waweze kutengwa na kulipwa na serikali.

Joseph Lokomol: *Ato mii shala nyo korom nyoman akushidan pooy, kewan 'ga Kapenguria.*

Translator: Kukiwa na mzozani ambao ni mkubwa zaidi ambao unaweza kuzidi kiwango cha hawa wazee. Anasema kwamba maneno haya irudi tu kwa hapa District ama wilaya tu isiendelee mpaka mbele tena.

Joseph Lokomol: *Tenoh chichan choni.*

Translator: Yake ni hayo.

Com. Lenaola: Asante Joseph. Councillor. Muruch Panjontok? Solomon Madanyang.

Solomon Madanyang: Basi asante sana. Kwa majina naitwa Madanyang' Solomon. Kwa hivyo ninashukuru sana kwa nafasi hii. Kwa hivyo mahali hapa kuna baadhi ya mambo ambayo mimi kama kijana naonelea ingefaa ipate kusikizwa.

Com. Lenaola: Tuna-record hii maneno na tukizungumza sana itapiga makelele tu. Kwa hivyo tunyamaze.

Solomon Madanyang: Kwa hivyo baadhi ya mambo ambayo ningependa zipate kusikizwa ni kwamba, katika Chila location mahali hapo tuna wazee ambao wanakaa mahali pale, kwa hivyo wale wazee tunaonelea ingefaa wapewe uwezo kwamba kama kuna jambo lolote ambalo kumetokea pale mtaani, kwa mfano kama kuna mgogoro mambo ya mashamba wale wazee wapewe uwezo ya kushughulikia ile mambo kisha serikali kwa njia ingine waweze ku work kitu fulani ama wawe wakiwapatia tuzo fulani kwa hiyo kazi.

Com. Lenaola: Sema tu walipwe.

Solomon Madanyang: Wapate kulipwa.

Com. Lenaola: Eeh, sema hivyo.

Solomon Madanyang: Ya pili, ningependelea kwamba katika kila wilaya pengine wilaya imegawanyika kwa constituency pengine tatu ama mawili ningependa kuonelea kwamba iwapo wale wote ambao watashinda katika Bunge kama ni wanaume na basi mahali pale ama kwa hiyo wilaya kama inawezekana mwanamke mmoja awe nominated.

Ya tatu, kuna mambo ya mazingara. Tunajua ya kwamba kama wakati huu serikali inatilia sana mkazo mambo ya mazingira.

Lakini tunaona wanaiimba tu mazingira, mazingira na ili hali hawawezi wakafika ndani kama upande huu, kwa sababu hawajatengeneza barabara. Kwa hivyo mimi naonelea kwamba wale wazee wa hapo, wapewe uwezo ya kutunga sheria yao wenyewe hapo. Na hata kamati wale ambao wanalipwa na serikali kutoka hapo hapo wapate kushughulikia haya mambo ya mazingira.

Ya nne, wale wazee ama tuseme katika kijiji ama location, tunajua ya kwamba kuna vile vitu kama madini, natural resources. We have the natural resources, so these natural resources the people of that area should have the responsibility about those resources. If it is forest or the issue of water down there. The people of that area should have the authority to say something over those issues. Because unasikia pale chini watu wanalalamika sana kwa sababu watu hawajachukuliwa kama wanaumuhimu ama serikali tu wanaonelea ama wenye wahahusika wanaonelea, wawo hawana sauti ya kusema kwamba tumeumia kwa sababu ya haya resources ama haya maji pale chini – Turkwell George.

Jambo lingine, tunapenda serikali wapate kushughulikia Wakenya wote, si eti wapate tu kushughulikia baadhi ya Wakenya. Kwa mfano, sehemu hii hata watu wengi wanashangaa sana ambao wanatoka juu wanasema kweli hapa ni Kenya. Kwa sababu hakuna barabara hakuna hospitali, hakuna hata mashule imejengwa. Kwa hivyo, mimi naonelea kwamba serikali ihakikishe ya kwamba Wakenya wote wanashughulikiwa kama ni barabara kila mtu awe na barabara. Ama barabara ifike kila mahali, kama ni hospitali, hospitali ifike kila mahali. Hii mahali pengine wanaweka lami kibahati bahati.

Jambo lingine, kwa mambo ya utawala wa mkoa. Tunaonelea kama, mimi naonelea pengine serikali ipate tu kuwachagua, lakini serikali ikiwachagua wawe wanapewa transfer kama watumishi wa serikali wengine.

Com. Lenaola: Hata DO pia, chief wote.

Solomon Madanyang: Mpaka assistant chief. Okay, kwa upande wa local government. Kuna watu ambao wanaitwa Mayor. Wakati huu tunaambiwa ya kwamba wao wanachukuliwa pengine baada ya miaka miwili wana renew na Chairman. Mimi naonelea hawo wapate kuchaguliwa na wananchi na awatumikie hata kuwa huo muda wote wa miaka tano.

Jambo lingine, Councillors. Councillors wawe ni watu ambao wenyewe wanajisimamia wenyewe kama watu wa Local Government. Wasiwe chini ya serikali.

Jambo lingine, yule mtu ambaye anatakikana kuwa Councillor, lazima awe amefika kiwango fulani cha elimu, kwa mfano form four. Hii ni kwa sababu.

Com. Lenaola: Pendekeza.

Solomon Madanyang: Jambo lingine, kwa upande wa lugha lazima awe anajua lugha zote kisawa sawa kama ni Kingereza na Kiswahili. Okay, ya mwisho mimi naonelea wananchi wapewe uwezo wakichagua Councillor wao leo na yule Councillor awatumikie kwa miaka miwili mitatu, na pengine watu hawajaona umuhimu wake wapate ku-recall ili election ifanywe na hii election ifanywe tu kama kwamba by-election imefanyika. Kwa hivyo ni hayo tu.

Com. Lenaola: Asante sana Solomon kwa maoni yako. Hatuna swali jilandikishe. Monica Lanyanga. Monica? Wale ambao niliita kitamba na hawakuweco nataka kujua ni nani ambao niliita na hawakuako. The persons that I called in the morning. Sema jina halafu endelea.

Monica Lanyang'a: *Kurenann Monica Lonyang'a.*

Translator: Jina langu ni Monica Lanyanga.

Monica Lanyanga: *Ng'alechan cho poh tagh.*

Translator: Jambo lake la kwanza.

Monica Lanyanga: *Atopan ng'alechai poh hospitali.*

Translator: Anasema kwamba anaunga mkono ma yale ya mbele ya hospitali.

Monica Lanyanga: *Acha yootun kikeghumionjecha nyoman.*

Translator: Anasema hawo kama akina mama wameumia kwa muda mrefu sana.

Monica Lanyanga: *Aku ombo lusiogh*

Translator: Hii zaidi kwa upande wa kujifungua.

Monica Lanyanga: *Mominye s'ptali korenchaa.*

Translator: Anasema kwamba sisi hatuna hospitali katika sehemu yetu.

Monica Lanyanga: *Ongu'nenan Ptoiyo location.*

Translator: Anasema yeye anatoka location ya Toyo.

Monica Lanyanga: *Oyoran kila location k'mii s'ptali.*

Translator: Anapendekeza kwamba kila location ipate kupata hospitali.

Monica Lanyanga: *K'ompo shida nu poh lusiogh.*

Translator: Anasema shida kubwa ni akina mama kujifungua.

Monica Lanyanga: *Nyoni nyo kesusecha nyoman.*

Translator: Anasema hiyo ndiyo shida yao kubwa zaidi.

Monica Lanyanga: *Ompo pich chole yootun.*

Translator: Kwa akina mama.

Monica Lanyanga: *Nyinii kechirr chii ogho.*

Translator: Anasema mama mjamzito akisikia uchungu ya kujifungua.

Monica Lanyanga: Eh *kukasa kichrr.*

Translator: Uchungu ukizidi.

Monica Lanyanga: *Monoh hospitali nyaa?*

Translator: Anasema sasa ni mashangao hospitali hakuna.

Monica Lanyanga: *Mii hospitalii wonii le Ortum*

Translator: Anasema huwa wanaenda hospitali sehemu ambayo ni mbali sana mahali pengine ambapo panaitwa Ortum – 160 kilometres.

Monica Lanyanga: *Nko Kapenguria.*

Translator: Anaongea juu ya sehemu bado anataka sehemu ingine ambapo panaitwa Kapenguria.

Monica Lanyanga: Miono *mt'kaa nyaa?*

Translator: Tena anasema kwamba pia shida ya barabara ama magari. Anasema kwamba pia shida ya barabara ama magari.

XX

Monica Lanyanga: *Keloh anapa tirkwa.*

Translator: Sasa hawo huwa wanashona kitu kama majela ya kuweza kuweka mtu juu yake halafu abebwe.

Monica Lanyanga: *Ketoh yoo tirkwa.*

Translator: Halafu yule mama anawekwa juu ya majela.

Monica Lanyanga: *Kepoh chepnyal, kite k'ma.*

Translator: Utapata kwamba kwa shida ya barabara na shida ya ubali ya hospitali utapata kwamba wamama wengi wanapoteza maisha yao kwa kuwa barabara hakuna na hospitali iko mbali.

Com. Lenaola: Basi pendekeza.

Monica Lanyanga: *Kigh nyoni nyo ko ng'wonje cha nyoman.*

Translator: Anasema kwamba hiyo ndiyo uchungu wetu mkubwa.

Com. Lenaola: Alikuwa amependekeza kwamba hospitali barabara

Monica Lanyanga: *Barabara nko hospitali.*

Translator: Pia barabara haiwezi kufika kila mahali pamoja na hospitali.

Monica Lanyanga: *Mokecha serikali k'tek hospitali keyichinocha korenyo.*

Translator: Anasema tunasikia kuna watu ambao wanaitwa serikali ambao walijenga sehemu zingine mahali kama Ortum, kama Kapenguria na mahali pengine. Na hawa serikali hawezi kutufikia.

Monica Lanyanga: *Koto kwich ne serikali?*

Translator: Anasema sasa hawa serikali kazi yao sasa ni nini.

Monica Lanyanga: *Ng'olionde anga napo.*

Translator: Jambo lingine.

Monica Lanyanga: *Ngala mutat.*

Translator: Pia angependa kuongea juu ya kupaswa kwa tohara ama kutairiwa kwa wasichana.

Monica Lanyanga: *Kamwachii loh kitorr yotunoh ng'ala mutat.*

Translator: Anasema kwamba kuna mtu alitaja kwamba akina mama ndio walianzisha jambo hilo.

Monica Lanyanga: *Kamuut monung' tolapai kumwah pich.*

Translator: Anasema kwamba wasichana wakitairiwa huwa wanatukana watu. Hilo ni jambo kutoka kwa wazee za zile.

Com. Lenaola: Hiyo ni kweli.

Monica Lanyanga: *Ng'ala kohny chonyi choh kikuluchchaa.*

Translator: Anasema hilo jambo lilikuwa nila zamani na lilikuwa linaingiliwa vile.

Monica Lanyanga: *Nyete le yee.*

Translator: Sasa basi anasema kwamba tumekuja kufahamu sasa shida zote ambazo huwa tunapata wakati wa kujifungua inatokana na kujifungua.

Monica Lanyanga: *Kokwochchaa loh kikampalalit ng'ala yuyo ompo mutat. Chona mochomoy nye ke muut kuroruchu walaka.*

Translator: Yeye anasema kwamba kuna wasichana wengi ambao wamejitahidi wanataka kubaki bila kutairiwa. Lakini kwa kuwa wengi walitairiwa basi wanapata hiyo aibu na wanaanza kuwa na nia ya kutairiwa.

Com. Lenaola: Wewe ungependa nini?

Monica Lanyanga: *Mochomanye ng'ala mutat.*

Translator: Anataka sasa kwamba kusiwe na kutairiwa kwa vyovyote ili isilete kwa hawa wengine ambao wanataka kujaribu.

Com. Lenaola: Sawa.

Monica Lanyanga: *Yoo nyo kanya katanyi.*

Translator: Anataka kusema kwamba mambo ya polygamy mama ambaye anatanguliwa kuolewa.

Monica Lanyanga: *Mokinoh yoo nyo tagh ketoh parenyi*

Translator: Anasema kwamba yule mama ambaye ataolewa kwanza apewe shamba lake.

Monica Lanyanga: *Nko tukuchi kila kitu.*

Translator: Apewe mali yake yote.

Monica Lanyanga: *Ompo achaa leh Pokoot..*

Translator: Kwa desturi yetu kama Pokot.

Monica Lanyanga: *Kipechaa yotun cho chang'.*

Translator: Desturi yetu ni kwamba huwa tunaoa wake wengi.

Monica Lanyanga: *Nya wow mokeyong'oy nye, tokang'n nyo poh lot.*

Translator: Anasema kwamba huyu mzee akianza kuoa yule mke wa pili ambaye bado ni mchanga, yule wa kwanza anaanza kutengwa mbali na mzee anaanza ku-concentrate kwa yule mdogo.

Monica Lanyanga: *Kighoy lonee ng'alechona angwanyi kochinan wow.*

Translator: Anasema sasa mimi ni mkubwa na yule mdogo ameolewa sasa tutafanya nini?

Monica Lanyanga: *Kikeprecha yootun nyoman. Ake nyagh nyona kochoru kuut.*

Translator: Anasema sasa shida ya kina mama tumenyanyaswa kweli kweli kwanza kwa viboko. Tumenyanyaswa yule ambaye anataka kutaja ataje nchi kiboko ndio hiyo.

Com. Lenaola: Kwa hivyo unasema nini?

Monica Lanyanga: *Kitoni chii tukuchii amominye chii nyo shalchinii chii tya, rupoy paat line ompo wolo mwoghecha lo rupoy ng'ala papo lenyini.*

Translator: Anasema katika district yetu kama Pokot huwa tunafuata mambo mzee akisha sema. Lakini hapa tungependa hii hali ya kusirutishwa kusiwepo. Kuchapwa na kupigiwa kelele ovyo ovyo.

Monica Lanyanga: *Omwoghan ng'la kirwokot, chai kakloh kutopoy kirwokot. Omwogha loh ketapa pchoni lenyoni.*

Translator: Amependekeza kwamba ameunga wale ambao walisema kwamba chiefs waweze kupiga mstari ama kupigiwa kura.

Monica Lanyanga: *Ato kumwa loh katap kumnee, mokino kuluku lenyini.*

Translator: Anasema kwamba ni heri ikiwa chiefs watachaguliwa iwapo akichaguliwa na wengi basi watakubaliana kwamba huyu ndiye tumemchagua na hakuna mwingine atasema jambo lolote.

Monica Lanyanga: *Tenoh choni chichan.*

Translator: Basi anasema yake ni hayo.

Com. Lenaola: Asante sana Monica. William Lomur? Hassan Baraza.

Hassan Baraza: Kile kitu ambacho kinanilazimisha kusimama mbele yenu ni upande wa kuabudu. Katika Katiba ya kwanza iliwasahau wale wenyeji katika kanisa, walijitoa mbele kutaka kumuabudu Mungu ipasavyo lakini igawa ni propaganda ya Mzungu kuwabandika mambo ambapo Mzungu aliwawekea kuwa ni dini ya uchawi. Na hata ya leo hiyo ni kitu imekuwa ni sugu katika wenyeji hawajawacha kufikiria yale ambayo Mzungu alikuwa akiweka. Sasa kwa hivyo katika Katiba hii tungelipenda mchunguze kwa makini mkiwa mnatakwishi mpate kufuata na kuingilia kuangalia, ili msije mkafunika vile wale wa kwanza walifunika.

Kitu ya pili, katika viongozi wa makanisa ambayo ilikuwako ya kwanza walishikwa na waliteswa na wakarudi wakawafanyishwa kazi na kunyang'anywa mali yao na mpaka wa leo walirudi wakawa maskini. Halafu dakika ya mwisho hawakuangaliwa kuonekana kama walikuwa ni binadamu bado Mzungu akawasongesha na ile mila na yale makosa ambayo aliwabandika ikaendelea kuwafinya na mpaka wa leo hawasikiki. Ndio kwa maana hata unapoangalia vile wako hapa saa hii kwa wakati wa leo wamekuja kwa mshangao kwa sababu umeona umevaa nguo ili waonekane katika mbele yenu, mjue ni kanisa hiyo political party. Na katika tangu mwaka wa elfu moja na mia tisa arobaini na nane hilo kanisa tangu lianzishwe mpaka wa leo, hakuna siku limepigana na serikali kama vile tunavyosikia Mungiki. Na pia hakuna jinsi wameingilia serikali pengine kwa mambo ya kisiasa. Na tunashangaa bado wakihitaji registration hawasikiki. Na wanapoenda kule wanaambiwa wangojee, sasa tumeshindwa ni Katiba gani ambayo iliwafinyia chini ambapo kuna kosa gani kubwa ambalo limefinya hii kanisa ambapo haisikiki. Tunataka kama nyinyi Tume muangalie muifungue iwe kama kanisa zingine. Kwa hayo machache sitazidi kuweka juu zaidi isipokuwa nitapeana hii karatasi kwa sababu inaandikwa kwa mambo marefu.

Com. Lenaola: Asante Bwana Baraza. Ningependa kujua hivi wakati kanisa ilianzishwa 1948 waka-apply for registration wakati wa Kizunguni, baada ya Kizunguni mli-apply registration baada ya independence?

Hassan Baraza: Ili-apply imekatazwa.

Com. Lenaola: Na imekatazwa. Okay. Tumeshukuru asante sana. Lumoreng Loitanyan. Kabla hujazungumza utazungumza vyote ama iko namna gani? Are you all giving views or want to present your memorandum? Okay, endelea.

Lumoreng Loitanyan: *Soroh out kikuchamu loh petoy pokotu kukiroy katiba.*

Translator: Anasema kwamba tumefurahi kwa kuwa ilikubaliwa kwamba kila mmoja anahusika katika marekebisho ya Katiba hata sisi ma-Pokot.

Lumoreng Loitanyan: *Kigh nyopoh tagh ku ng'ala masomo.*

Translator: Jambo la kwanza angependa kuongea juu ya masomo.

Lumoreng Loitanyan: *Omokan pich cholenye acha , cho motung ' nye title deed keto masomo nyopoh k'le.*

Translator: Anasema kwamba tunaona kwamba watu walipendekeza kuwa elimu iwe ni ya bure na tunajua jambo la bure huwa ni asifi na amependekeza kwamba watu ambao hawana title deeds katika mashamba zao watoto wao waweze kusomesha free.

Lumoreng Loitanyan: *Ata tomo kunyoru chi title deed ku parenyi mpaka tooh.*

Translator: Anasema kwamba huwa tunaambiwa kwamba mtu ambaye hana title deed hana mamlaka juu ya shamba lake. Lakini tunasema kwamba kuwekwe title deed ama kusiwekwe shamba bado nila mwenye shamba mpaka chini.

Lumoreng Loitanyan: *Mokechaa skul nyole secondary nyopoh tip'n nko nyo poh werko, nyo somonoy monung'o klee.*

Translator: Anapendekeza kwamba elimu ya shule ya upili iwe niya bure kwa sisi wa-Pokot.

Lumoreng Loitanyan: *Tokusoman monechaa cho chreroch. Ompo wolo yee kepotcho monee chaa cho chreroch.*

Translator: Anasema kwamba hii ikuwe kwa upande wa wavulana na wasichana na ni kwamba watoto wetu wamerudi kutoka mashule na wamerudi kukaa nyumbani wamekuwa tu wajinga kwa sababu hawakuendelea na elimu yao kwa ajili ya karo.

Lumoreng Loitanyan: *Tich opun chinii kupoghisyechaa, mominye pikochaa choh kis'k kasiin.*

Translator: Anasema sisi kama Pokot huwa tunategemea sana ng'ombe kwa jili ya karo na tutapata kuendelea sana.

Com. Lenaola: Apendekeze juu ya ng'ombe na

Lumoreng Loitanyan: *Ng'ata arawa akong'a mpaka nyopoh nane, mominye wolo kiolteho tich, mii ng'uny bei. Memukoh nyee monung'o school.*

Translator: Anasema sehemu yetu hii sanasana wakati wa kwanza hadi mwezi wa nane huwa bei ya ng'ombe inarudi chini sana na soko zetu huwa si steady sana na huwa tunapata shida sana kusomesha watoto wetu.

Lumoreng Loitanyan: *Ng'la kansalen yee nyu.*

Translator: Anaongea juu ya Councillors.

Lumoreng Loitanyan: *Prichinechaa kura kansla nyo ngut kukiroy akusoman..*

Translator: Anasema kwamba kwa upande wa Councillors tunataka mtu ambaye anaweza kusoma na kuandika.

Lumoreng Loitanyan: *Ompo acha wolo poroh mominye skul nyo kiketek, mengut nyee pich kukiroy.*

Translator: Anasema sasa sehemu zetu za ndani sana huwa hatuna shule ambazo zimejengwa kule.

Lumoreng Loitanyan: *Ato kiyar kansala nyo kikusoman , mo kis'kecha nyee kansala.*

Translator: Anasema tukichagua madiwani ambao wamehitimu elimu ya juu itakuwa ni kwamba sehemu zetu sasa ambao hatuna watu ambao walisoma hatutakuwa na Councillors wowote. Na ili kwamba itabidi watu watoke mbali kuja kututawala ambayo ni ngumu.

Lumoreng Loitanyan: *Mutat nyo poh tip'n.*

Translator: Kutairiwa kwa wasichana.

Lumoreng Loitanyan: *Mi pich cho ngut loh ato kumuut tip'n kuchundoy, mengut nyee pich cho mi wol le har.Mominye ketoh lasma ng'ala mutat nyo poh tip'n .*

Translator: Basi huyu amekana ile hoja ya watu kwamba ya kuhusu kutairiwa kwa wasichana iwekwe huru. Wale ambao wanataka kutairi wasichana wao wafanye vile. Na wale ambao wana amini kwamba kutairiwa kwa msichana kunamfanya awe mjinga basi wakomeshe.

Lumoreng Loitanyan: *Mokechaa kutang' tagh n'gala tilyantan ompo tich.*

Translator: Anasema kuna pia desturi ya uhusiano kwa ng'ombe. Mtu akikupea ng'ombe huwa anafuata wakati fulani kuja kukuuliza kama ng'ombe wake aliendelea namna gani halafu achukue. Anasema kwamba hali hiyo pia iwekwe huru wenye wataendelea kufuatana wafuatane wenye hawataki kufuatana pia wakatishe.

Lumoreng Loitanyan: *Ng'la kirwokot.*

Translator: Mambo ya chiefs.

Lumoreng Loitanyan: *Mokechaa ketap kirwokiin. Wongoy interview ropiyen.*

Translator: Anasema kwamba chiefs waweze kutungwa mlolongo kwa kuwa kama itakuwa ni interview basi watu wengi watapoteza pesa mara kupeana hongo mara kwa apply na labda baadaye hawezi kupata hiyo kazi.

Lumoreng Loitanyan: *Ambaye amechaguliwa afanye kazi yake mpaka retire.*

Translator: Basi anataka huyu mtu apigwe mlolongo na afanye kazi akishindwa kuchaguliwa mpaka apigwe retire.

Lumoreng Loitanyan: *Ato igh makosa, kefutancha aketap anga.*

Translator: Anasema kwamba huyu chief akipatikana na kosa lolote, sisi kama wananchi ndiyo tunakuwa na mamlaka ya kuweza kumfuta.

Lumoreng Loitanyan: *lenye pichu le MPs. Mokinoh nyo kikwit form four kutook.*

Translator: Anasema kwamba hawa waheshimiwa ama MPs anasema kwamba mtu ambaye amehitimu kiwango cha kidato cha nne ndiye anaweza kuchaguliwa kuwa mbunge.

Lumoreng Loitanyan: *Ato igh makosa kewirta tomoh kwit mwakeni chai le muut.*

Translator: Pia anasema kwamba hapa tupatiwe nafasi ya kuweza ku-recall akitenda kosa lolote hapa katikati vote of no confidence pia iweze kuwekwa pale, halafu aweze kurudishwa nyumbani.

Lumoreng Loitanyan: *mokecha president kwip ng'alechi bunge, mochomechaa nye nyo ighoy ngalechii ongut.*

Translator: Basi anaongea pia kuhusu serikali kuu haswa yule Rais. Anasema kwamba huyo anahitajika kwenda katika Bunge aweze kutoa hoja zake mipango yake yote iweze kusikika kule. Isiwe ni kwamba mipango ya pekee ambayo anapanga peke yake.

Lumoreng Loitanyan: *Mominye ng'lechai mutoi mwakeni pitagh poh rais.*

Translator: Basi anasema kwamba kusiwe na retire ya president. Ikuwa kama mtu angali anaweza aendelee na anaongea juu ya mambo ya kura. Kusikuwe na ile ya kusema kwamba mtu anapigwa kura two terms halafu anakaa. Anataka kama bado mtu anawesa aendelee.

Lumoreng Loitanyan: *Teehn*

Translator: Basi amefika mwisho.

Com. Lenaola: Asante sana Loitanyan jilandikishe pale. Yuwaring Ameme.

Com. Lenaola: Sema jina halafu endelea.

Yuwaring Ameme: *Kurenann Siwareng Amemee, korenyan Tamugh.*

Translator: Anatoka sehemu ya Tamugh.

Yuwaring Ameme: *Soroh pipo tume ompo wolo katukwa wol keross katiba.*

Translator: Basi anashukuru Tume kwa kuweza kuja huku kuleta mambo ya Katiba.

Yuwaring Ameme: *Ompo wolo keghun ktterr kompolelut chopoh ptang 'eng' mot toh kung 'arach.*

Translator: Anasema kwamba sasa imetufikia ili iweze kusikia shida zenu zote ili iweze kutusaidia.

Yuwaring Ameme: *Mokinoh kewagh tororot, tolopai sheria nko poytogh'. Mii poytogh'o ng 'unyi sheria, melo wolotoo.*

Translator: Anasema kwamba maneno haya matatu yapangwe hivi. Mungu awe mbele, Katiba halafu kiongozi.

Yuwaring Ameme: *Aregistana ng 'ala tororot toh kwit korr lowurr.*

Translator: Basi anasema kwamba kikao hiki walikuwa wamesema maneno mengi na pia angependa kusema kuhusu mambo ya dini ili neno la Mungu liweze kuenea kila mahali.

Yuwaring Ameme: *M rokononyee kupurchu katiba ng 'olyonto tororot ng 'uny.*

Translator: Basi kulingana na shida hajaanza kwamba Mungu mbele, Katiba halafu kiongozi anasema hasa kwamba sisi kuna sheria ambayo imefinyia sasa neno la Mungu chini. Kukataa makanisa mengine iendelee. Basi imegeuga ile mpango wake wa kusema kwamba Mungu kwanza. Na Katiba hata imekuja juu ya neno la Mungu.

Yuwaring Ameme: *Toh kwamta pasta ngo'lyonto tororot korr k'mukul.*

Translator: Ili sasa muhubiri apate kueneza neno la Mungu kwa dunia nzima.

Yuwaring Ameme: *Soroh kusoyonisho ng'ale chona. Mokino ropiyeni koltin keparr k'nyul somok;contractor, chipo parr nko serikalai.*

Translator: Kwanza anaongea juu ya madini ambayo inapatikana katika mashamba yetu, anasema kwamba igawanwa mara tatu ikuwe ikifanywa mara tatu, kwa contractor na mwenye shamba pia na serikali.

Yuwaring Ameme: *Makulut ng'alechu kamwgha yii pr'nda.*

Translator: Basi anasema kwamba ni wazo kwa Tume kwamba waweze kuzingatia maneno yetu yote isikuwe kwamba tunasema tu.

Yuwaring Ameme: *Kitoa nga, chomecha ng'ala jimbo.*

Translator: Basi yeye pia anapendekeza uongozi wa majimbo.

Yuwaring Ameme: *Mamlaka nyopo paitagh nyo wow mpaka mkasa, mokoy ke kul mkasa. A kulipan serikali mshara.*

Translator: Basi anaongea juu ya mzee wa mtaa ambaye anajulikana sana kwa jina “Makasa”. Na anasema kwamba huyu mzee ni lazima pia apige kura na pia apate mshahara kutoka kwa serikali.

Yuwaring Ameme: *Karam ke proy kura kirwokot. Sosohoi chii man ompo wolo mokoy asiyech kupaita napoo.*

Translator: Tunaamini kwamba chiefs wakitungwa mlolongo tutaamini kwamba watafanya kazi yao kwa njia nzuri sana kwa kuwa atakuwa akichunga ili aweze kurudishwa mamlakani tena mara ya pili.

Yuwaring Ameme: *Ata ketung'etecha korenyo. Mokecha tume kusuwa loh mikorencha Kitale wolo naa. Kiyonecha*

musungun, konyi kwenda. Morecha korenja.

Translator: Basi pia anaongea juu ya shamba la Pokot ambalo limetengwa. Sasa wana-claim kwamba kuna shamba letu ambalo limechukuliwa hapo awali na Wazungu na limetengwa na vile warizurutishwa na Wazungu kufukuzwa upande huu, shamba hilo likamilikiwa na watu wengine ambao wanatoka mbali. Basi anasema kwamba jambo hilo liwezwe kuingizwa kwa Katiba kwamba shamba la wenyewe liwe lao.

Yuwaring Ameme: *Ono wolo kikurochu porwoi pipo mafuta pole cho kirata kolowo. Miono prumboti?*

IDs: Mambo ya vitambulisho tunataka watu wenye wanatupatia vitambulisho wakuje kila location. Na hatutaki hiyo maneno ya kuambiwa eti ulizaliwa wapi. Mimi najua nilizaliwa nyumbani hata pengine sina card ya hospitali, hata sikuenda kanisa. Mamangu hajui kanisa enye ningeambiwa ulizaliwa huko na baptisim card. Sina. Ninaambiwa niende next week and sisi tuko na ma-centre moja moja. Tulienda centre mara moja kama sasa Chepkobe tuna Tuesday peke yake. Ukienda hizo siku zingine huwezi pata mtu. Sasa mpaka Tuesday. Na kama mimi sasa nataka kwenda kazi nitatoa hiyo mambo yote ya vetting, unaulizwa nini, babako ni nani, nani, nani?

Mambo ya midwives: Kama mahali kama hapa tuna population kwa sababu wengine wanaoa wanawake wawili, watatu na hawa lazima wanazaa. Na kuzaa ni nyumbani na kuna wenye wako na problem ya kuzaa. Kila mtu hatuko sawa. Kuna mtu anaweza zaa vizuri na sasa tunataka wale wamama wamekomaa, wenye wamekomaa wapelekwe hiyo college vile wanazalisha mtu. Na wapewe hiyo instruments, mtu akishindwa kabisa kuzaa ajue vile atamsaidia. Na tunataka ikuwe karibu pande hii, kuliko kwenda mbali Kapenguria.

Mambo ya Tax: Kama sasa watu wa County Council unaona mtu anakunywa mpaka kwa duka, ama soko. Mimi nauza nyanya, nimepata shilingi tano zangu nikuje saa mbili mpaka saa tano niko na shilingi tano. Mtu wa County Council anakuja kuniambia leta shilingi thelathini. Sasa nitatoa wapi thirty bob saa hiyo, sina. Niko na shilingi tano, unaona anaanza kumwaga nyanya kama ni nini makuku zinatawanyika eti kwa sababu umekataa kutoa hiyo kodi ya shillingi thelathini. Na hawezi kukupatia muda.

Free education: Wasichana tunataka kusoma. Na kuna wazazi ambao wanasema wasichana hawasoma. Mtu ameweka vijana wake wote kwa shule. Ng'ombe inauzwa ni kijana tu, shamba inauzwa ni kijana tu. Sasa sisi tunataka msichana asome na kama mimi ni mwalimu niambie mtoto, mtoto enda kwa chief enda useme mwalimi ameniambia baba amenikataza shule. Mimi nataka chief achukue hatua, aende astaki huyo baba, hata kama ni baba yangu aende amstaki. Kwa sababu anaweza kataza aje msichana asiende shule. Kwa sababu mtoto akiongea atapigwa. Mtoto akiongea atapigwa ama amuambie nitakunyonga. Sasa sisi tunataka ndio tusinyongwe aende kwa chief, chief aongee na baba kabisa. Pia na vitabu. Vitabu viwe ni free, kama ni dormitory kitanda iwe mattress free and iwe tu niya usafi, hata kama huku ni wa-Pokot tunataka pia tukuwe wasafi. Mimi sina mengi ni hayo tu, asante.

Com. Lenaola: Thank you Margaret. Njoo ujiandikishe hapa. Mathew. Baada ya Mathew ma-chief.

Mathew Moria: Kwa jina ni Mathew Moria. Mimi pia ningetaka nitoe maoni yangu kama mtu binafsi. Niko tu na maoni machache. Moja ni kuhusu mahakama – ningeonelea hivi kila Mkenya apate nafasi ya kufikisha mambo yake kortini. Kwa sasa ni ngumu sana, penye tuko hapa na Kapenguria ni kitu kama kilometre sabini, kortini huko ni mbali na ni kazi ngumu hongo katikati na kadhalika. Tunaonelea hivi njia moja rahisi ni kwamba kuna jamii ziko na njia ya kutatua mizozo, migorogoro na kadhalika kama ya ki-Pokot. Nashukuru kwamba watu mmeongea hapo mbeleni kwamba kuna hii ya Pokot tungetaka iendelee. Kwa hivyo tungetaka kwamba katika Kenya hii kama kuna jamii ambazo wako na njia ya kutatua migorogoro kwa njia rahisi iwekwe Katiba na Katiba itambue kama vile na kadhalika. Hilo ni pendekezo yangu kwa mambo ya mahakama.

Kuhusu Local Authorities: Ningetaka kusema tu mambo mawili hapo kwamba mayors na chairmen wachaguliwe moja kwa moja na wananchi. Na hiyo itakuwa ni baaba ya uchaguzi, kwamba baada ya Councillor fulani amechaguliwa na angetaka pia kuwa Chairman, nafasi ya kuchagua sasa Chairman wa muda itatengwa kwa jili ya shughuli hiyo – Chairman na Mayor. Pia mishahara ya Madiwani ilipwe na serikali kuu kama wale wengine. Na mishahara huyo pia uwe mnono kiasi kwamba kwa sababu hawa ndio wanawakilisha wananchi moja kwa moja, mishahara iwe kiasi ambayo hawa watapata nafasi ya kuhudumia wananchi. Hiyo ni kuhusu mambo ya Local Authorities.

Electoral System: Mambo ya kuchagua Councillor, Mbunge na President wakati mmoja naonelea kwangu kwamba si mzuri. Shida inaweza kutokea namna hii, President wanaweza kuwa wanang'ang'ania kiti na wakati huyo matokeo ya MP, ya

Councillors ndiyo hiyo, nchi inaweza kuingia kwenye janga kubwa sana. Kwa hivyo tuchague President wakati wake. Halafu Parliamentary na Civic wakati wake tofauti, labda kwa mambo ya costs tukitaka kupunguza. Ili nchi isije ikagonga ukuta kwa mambo ya janga kwamba President wanang'ang'ania kiti pale kama vile Sri Lanka. Nani atachunga nchi wakati huo. Kwa hivyo President achaguliwe wakati wake, Wabunge na maCouncillors wakati wao, ili nchi iende polepole.

Pendekezo langu la nne, ambalo ni mambo tu madogo madogo ni kwamba yule anaitwa Registrar of Societies, yule mtu anasajili muungano ya watu hapa na pale iwe katika ngazi ya wilaya. Watu wa Mafuta Pole wamelalamika kwa sababu wanaenda Nairobi wanaambiwa sijui kuja kesho imekuwa ni ngumu, ingekuwa ni hapa Kapenguria hiyo shida ingekuwa imekwisha kwa wakati wake.

Mambo ya Provincial Administration, ningependelea tu kwamba iendelee lakini bureaucracy yaani iko chain mrefu sana, Assistant Chief, Chief, DO, DC, PC, President ningetaka short-cut kidogo. Na hii ndio pendekezo langu, hakuna mtu anaitwa Assistant Chief badala yake anaitwa Chief. Halafu hakuna sasa Chief yule tuko naye saa hizi, ni Chief yule ameenda kwa Sub-Location. Halafu hakuna DO tuko na DC. Halafu President. Hii inakuwa short-cut namna hiyo kwa sababu hatujui kazi ya DO saa hizi ni nini, hatuoni. Wanatumia tu machiefs saa hizi, kwa hivyo Chief awe na mamlaka kamili ile kazi ya DO iende kwa Chief. Halafu wananchi wapate mambo ya utawala iwe karibu, sasa hii apana iko karibu. Mpaka upitie hii, hii inakuwa ni kazi ngumu.

Mambo ya Title Deeds: Hatujui ni kwa nini serikali imekawiya sana. Kabla mimi sijatoa maoni hapo mnaona kama wananchi kwamba labda ni njama. Kama hapa Sok tangu mwaka wa sabini na mbili miaka thelathini iliyopita watu wamejigawia mashamba lakini hakuna title deeds mpaka saa hizi. Labda ni kwa sababu wanasema serikali labda kitu ikipatikana hapo wakuje wanyakue ama nini, kwa hivyo kuanzia sasa kuenda mbele tungetaka hiyo mambo ya title deed iwe haraka kabisa iwezekanavyo. Halafu watu wazalishe mali badala ya kugombana kuhusu mambo ya ardhi. Pia kuhusu mambo ya chakula serikali napendelea hivi Katiba ipee mamlaka serikali ihakikishe kwamba food security kwa nchi iko. Nchi kama Kenya hatutaki kuombwa ombwa chakula kila wakati tunaonekana kama ni maskini. Serikali ingejua kutambua kwamba mwaka huu tuko na kiasi ya chakula kiasi hii, kwa hivyo ipange hata angalao ya miaka tano tusije tukapata shida kila wakati.

Pia, mambo ya kupendelea wanawake katika Katiba ningependelea hasa katika mambo ya utawala, vyeo, siasa. Kwa sababu tunasoma kwa pamoja, shule ni ya wasichana na wavulana. College ni moja, halafu wakati wa kazi tunasema hapana wanamume chini mwanamke juu, sijui kwa nini. Tunataka kusema hivi, wang'ang'anie kwa usawa, kila mtu na qualification yake. Kwa sababu walisoma kwa mambo ya usawa. Lakini kunyanyasa wanawake sipendi.

Haya ningesema pia free education for all. Yaani elimu iwe ni bure. Yaani serikali ikarimie sio bure vile, ikarimie elimu kuanzia nursery mpaka form four, halafu labda chuo kikuu kwa sababu gharama itakuwa juu serikali ichangie. Halafu ningependelea hivi, baada ya Katiba iwe tayari tusema kwamba tuanze mpya kwa sababu hii itasaidia nchi yetu itainua uchumi na mambo mengi tuweke miaka ishirini. Hii mambo ya free education halafu baada ya hiyo miaka tunatarajia nchi hii itakuwa imebadilika

na uchumi itakuwa imekuwa bora, kwa hivyo hapo ndio tutaweza kubadilisha hiyo sehemu hiyo.

Com. Lenaola: Jambo la mwisho. Second last.

Mathew Moria: Second last. Ningependelea hivi watu ambao wanataka kuwa machiefs in future, waanze na college. Mtu ana-apply tu kuenda college halafu anahitimu kama Chief halafu nafasi ikitangazwa analeta Chief yake. Kwa sababu saa hizi imekuwa ni jambo la kienyeji iko nafasi hapo halafu anapewa mamlaka nyingi, Chairman wa security, maendeleo na hataenda course ya hiyo, kwa hivyo atangulie na course.

Ya mwisho, ni kwamba kazi ya wanasiasa na watala ijulikane wazi. Saa hizi hatujui kazi ya MP ni nini, sijui ni harambee peke yake. Hatujui ya Councillors, kwa hivyo tungetaka iwe well defined kwa Constitution mpya kwamba kazi ya MP ni hii, kazi ya Councillor ni hii, kazi ya Chief ni hii na wananchi wajue ndio maendeleo itakuwa haraka. Natarajia Tume hii itatupatia heshima kama taifa la Kenya na tutaendelea mbele vizuri. Asanteni sana.

Com. Lenaola: Asante sana Mathew kwa maoni yako. Chief?

Simon Olerup: Majina yangu naitwa Simon Olerup ni Chief wa hapa Sop. Niko na machache ya kusema kwa Katiba. Ningependa kusema tu tuwe na matibabu ya bure na pia tuwe na elimu ya bure kutoka darasa la kwanza mpaka university. Pia ningesema Wabunge mishahara yao ipunguzwe ili maCouncillors wanao wengi kabisa tuko na thamanini kwa West Pokot wapate mishahara nyingi kutokana na mkato ile ya Wabunge. Na Councillor awe mtu ya form four, kwa sababu akiwa mtu wa form four ikiwa pesa itakuja ya Council kwa sababu sasa tumesikia kwamba kwa mwaka moja tunapata karibu milioni. Lakini siju inafanywa namna gani pale Kapenguria haifiki hapa kwa sababu wale maCouncillors wako huko hawajui hata kazi ya Council yenyewe ni kitu gani. Kwa hivyo Councillor ikiwa atachaguliwa yule amesoma, wapewe seminar pia wajue namna ya kufanya kazi ya Council. Councillor ajue Council ni nini, asifike kwa location tu aanze kubadilisha na Chief. Chief anajaribu kupanga hii, Councillor anasema si hii ni namna hiyo, ili apate kura kesho yake. Kwa hivyo tungetaka Councillor apate pesa sio chini ya elfu hamsini. Na wafanyikazi wa serikali waweze kuenda retire wakina na miaka sitini. Kwa sababu ukiona mimi saa hii unaona kama ni kijana, niko na miaka karibu arobaini, inabaki kumi tu. Kwa hivyo ningesema kwamba ikiongezwa iwe sitini mtu anafanya kazi mpaka amekomaa kabisa. Mlisikia saa ile watu wanapendekeza kwamba mtu awe miaka thelathini, sasa akifanya karibu mwaka thelathini hiyo tena atafanya kazi ya muhimu.

Na kwamba mambo ya msitu mara nyingi kuna shida. Tuko na mambo ya msitu na sasa ile unasikia Chief ni Chairman ya kila kitu kwa location. Lakini kidogo unaona mkubwa wa forest unaona mara askari ya forest iko hapa anataka kusema mimi ndio najua mpaka ya forest ni hapa na pale. Tungesema na kidogo hivi tunasikia kuna yule mkubwa kabisa, kwa serikali ni conservative..... Sasa huyu amepewa mamlaka nyingi sana kuhusu mambo ya msitu, tungependa Chief awe na kamati yake katika location ya kujua mpaka ya forest ni hii na tukisema tuchunge namna hii Chief awe na mamlaka kamili. Akishika mtu ashtakiwe atibiwe kamili kwa sababu saa hii tukipeleka mtu Kapenguria anapigwa fine shilingi mia moja hamsini. Na ni mtu

mwenye aliyeharibu forest, si atarudi kesho yake huko. Na pia tuko na wazee wenye wanatusaidia katika kazi zetu. Sheria imetupatia wazee ya kusaidia sisi kutoka sub-location mpaka location. Tuko na wa division pia, lakini wale wa location mimi ningependa hivi, wananchi wenyewe wachague hawa. Baada ya miaka tano wanabadilishwa na hawa wazee wapewe uwezo zaidi, badala ya ile makosa ikifanyika kwa location inanzia kwa wazee, hata kama itaenda kwa polisi baadaye, ionekane kama imeshinda wazee ndio iende sasa kortini. Na hawa wazee pia wapewe allowance kidogo, na hiyo allowance inatokana na wale wako na makosa na serikali pia waongeze kidogo ili wapate mshahara ya kila mwezi. Wasiwe tempted kwa kutaka kiinua mgongo ili asaidie mwingine.

Watu wamesema kwamba kazi ya Chief tupige kura. Mimi ningeaona hiyo ikiwa hatutaogopa kufanya hiyo kazi ama tupige kura, lakini mimi najua kazi itaharibika kwa sababu nitajitetea kupata kura. Sasa watu wakikosana wawili mimi naona pengine ni yule alinisaidia kufanyia mimi campaign, sitafanya haki hapo. Kwa hivyo hiyo kazi ikipigwa kura hakutakuwa na uamuzi kamili.

Com. Lenaola: Ungependa mkae vile mko sasa?

Simon Olerup: Sasa kwa hivyo ningependa tukae vile tuko sasa. Na mambo ya uwezo ya President. Sasa hivi watu wanasema kwamba President pengine ako na mamlaka nyingi ipunguzwe. Kwangu mimi ningependa kwamba hiyo uwezo ikae vile iko, kwa sababu mtu akiwa kwake, mimi sasa nikiwa kwangu na isemekana inaonekana hiyo uwezo ipewe bibi yangu awe na uzito karibu sawa na yangu, hiyo boma itakuwa na mashindano. Kwa hivyo ningependa President awe na mamlaka yake kamili, vile ako nayo sasa.

Com. Lenaola: Mbili ya mwisho.

Simon Olerup: Ikiwa tutakamata watu kutoka location, angalau tupewe ruhusa kidogo ya kutafuta gari, kwa sababu saa hii tunaambiwa tusikae isizidi masaa ishirini na nne. Tungependa sasa iangaliwe umbali, kama ni Chepariya huko itakuwa ni sawa, hata kama ni ten hours ni sawa. Lakini ikiwa Sop hapa iongozwe hata mpaka siku mbili, kwa sababu hakuna gari na unaona mtu ni mkosaji hatuwezi kuwachilia. Tuogope sheria kwamba tusikae na mtu masaa ishirini na nne. Kwa hivyo tungependekeza hiyo ikae mpaka wakati huo. Na pia ikiwa tumekamata mtu kutoka location, hapo Kapenguria tungeomba huyo mtu yule amebaki muda mfupi aletwe hapa ili asaidie kazi ya community katika hapa.

Jambo la mwisho, tuko na NGOs. Unasikia NGO amekuja na pengine milioni ishirini kufanyia kazi Sop hapa, na dakika ya mwisho inaona ile kazi wamefanya haijafika hapo, kwa sababu ya mishahara na ma-allowances mingi mingi. Tungependa iwe 10% peke yake ndio watafanya kwa hiyo kazi ingine na pesa yote ikuje isaidie yule mtu alikusudiwa kusaidiwa. Kwa hivyo ningesema ni hayo tu.

Com. Lenaola: Asante sana mzee.

Com. Yano: Jiandikishe jina.

Com. Lenaola: Jonathan Anupa. Halafu Ngoriakang Ndumurei. Wapi yeye?

Jonathan Anupa: Thank you very much the Commissioners.

Com. Lenaola: Sema jina halafu endelea.

Jonathan Anupa: My name is Jonathan Anupa and here are my views.

- (1) About the date of election: The date of election should be stated in the current Constitution to avoid tense and confusion.
- (2) Local Government: The Mayor and the Chairman of any given Municipal Council should be elected by wananchi to serve all the people.
- (3) The Councillor: The lowest level of the Councillor should be a form four and that of the Mayor should be also above form four. Councillors' salaries should be passed in the Parliament and financed from the Government Treasury, because you find most Councillors are very poor, such that they cannot even afford transport.
- (4) The current Constitution should limit the powers and the functions of the President e.g. the President should not have powers to appoint Vice President, Ministers, Ambassadors, etc instead they should be elected by the Members of Parliament.
- (5) The salary and allowances of Members of Parliament should be decided by the wananchi or courts to avoid huge demands of the same without considering the economy. You find most of these MPs are demanding a lot of salaries and yet they don't consider the economy.
- (6) We should have a Prime Minister who is selected by wananchi and instead of President should only be ceremonial.
- (7) The opposition parties should be financed by the public funds, because they represent and the people pay taxes to the Government.

(8) The President should remain the Commander-in-Chief of all armed forces, because his office is in charge of maintaining peace and unity in the country.

(9) Any person found to have stolen public money e.g. for example 100 million should be fined equivalent amount of money and sentenced for four years to serve as an example to others, hence avoid corruption.

Thank you very much.

Com. Lenaola: Thank you Jonathan. Gurekang' Domoren.

Gurekang' Domoren: *Otepan kigh akong'a nyo tong'oh.*

Translator: Anasema anauliza jambo fupi tu si kubwa sana.

Gurekang' Domoren: *Kamwagha kwa atai ng'ala monung' loh momutonye, wolo poh kony.*

Translator: Anasema kwamba mliongea juu ya kutairiwa kwa wasichana, lakini jambo hili lilikuwa na jambo la awali sana.

Gurekang' Domoren: *Kochi nyole sapana.*

Translator: Basi kunakuwa na sherehe ingine kwa Pokot ambayo inaitwa "Sapana".

Gurekang' Domoren: *K'noghecha korka tomominye chi nyo long'oy kookai.*

Translator: Jambo la tatu ni kwamba mke huwa anapewe pete ya kuonyesha kwamba ni mke wa mtu.

Com. Lenaola: Angetaka nini juu ya tohara?

Translator: *Yarenyi lonee ombo mutata monung'?*

Gurekang' Domoren: *Oyoran kemut.*

Translator: Basi anataka kwamba wasichana waendeleo kutairiwa.

Gurekang' Domoren: *Mopustonye chi Sapana kookai.*

Translator: Anasema kuna sherehe ingine inaitwa "Sapana" kwamba its an initiation ceremony to pass into manhood.

Anasema kwamba hiyo pia iendelee.

Gurekang' Domoren: *Serikali choleng'oo nya wey?*

Translator: Anauliza hii Katiba ni kama ya hapo awali ama ni ingine ambayo imekuja sasa?

Com. Lenaola: Ni mpya.

Gurekang' Domoren: *Ng'o nyu kiyotu ng'alechu mutoy korr? Kesh pich kchop paren.*

Translator: Anasema kwamba ni nani ndiye alileta hii hoja ya kusema kwamba mashamba inagawanywagawanywa, na imefanya watu wengi wamebaki bila mashamba.

Gurekang' Domoren: *Melokimi korenchaa!*

Com. Lenaola: Angependa nini?

Translator: *Ii yorenyi lohnee?*

Gurekang' Domoren: *O Moran serikali ku yorwanun parr!*

Translator: Anasema kwamba sasa mimi sina shamba serikali watanifanyia nini na watu wamegawa mashamba wamechukua?

Com. Lenaola: Ungependa nini?

Translator: *Yerenyi lohnee?*

Gurekang' Domoren: *Oyoran serikali kusorwanun.*

Translator: Basi anataka serikali imuokoe kwa kutafutia shamba.

Com. Lenaola: Haya jambo lingine.

Translator: *Ng'olyonte anga.*

Gurekang' Domoren: *Mii parenyan wono le Kapkai.*

Translator: Anasema kuna shamba lake huko mahali ambao panaitwa Kapkai.

Gurekang' Domoren: *Nyo kiyona pich serikalii loh kwenda kwenda!*

Translator: Anasema kwamba kuna shamba lao liko pale panaitwa Kapkai ambapo walifukuzwa hapo wakati wa Mzungu, waliambiwa kuenda. Walitumia neno hilo kumanisha kwamba watoke sehemu hiyo. Basi anasema sasa anataka shamba hilo lirejelee kwao.

Gurekang' Domoren: *Omoran korenyu! Mominye anga.*

Translator: Anasema hana mengine ni hayo.

Com. Lenaola: John Mukal? Is that John? Na naona saa imekaribia kwenda, kwa hivyo tafadhali nikikuita kuja point, point, point na kwenda ndiyo tumelize kila mtu.

John Mukal: Kwa majina naitwa John Mukal. Ninazungumza juu ya elimu. Elimu iwe ya bure kwa watoto wote kuanzia pre-primary mpaka secondary. Kwa madarasa wakati ilianzishwa 8-4-4 yaani iweko na darasa la nane ilifanya watoto wengi wakakosa kazi. Sasa tunataka iwe na darasa la saba kama zamani kuanzia pre-primary mpaka class seven. Na isiwe na mtihani ambao watoto wanafanya wakiwa kwa primary, kwa sababu unakuta watoto wanarudi kule nyumbani, kwamba wameanguka mtihani. Kuanzia wakati mtoto anapoanza shule katika pre-primary, primary level mpaka class seven, iwe inatumika ile assessment tests and inapitisha huyo mtoto kuenda form one na kuendelea. Wakati anapoenda form four apana soma subjects yote. Ana-specialize kwa subjects fulani na anapeleka mpaka wakati anamaliza form four ndio atafanya mtihani na iwepo na form five and six halafu anaenda university. Kwa sababu wote wamesongamania mahali pamoja.

Halafu pia, kwa upande wa educational structure or administration. Tunataka tumeangaika waalimu zaidi, kwa sababu tunaambiwa unatakikana kuenda TSC huko Nairobi. Inatakikana TSC ile final TSC inakuja kwa district level . Na ukikuta ya kwamba kuna officers wengi wamechukua pesa za serikali wengi wanakaa katika ofisi ya education, iwekwe tu na District Education Officer na makarani wake na isiwe na mtu ambaye anaitwa Divisional Educational Office. Iwe tu na Zonal na Sub-location Planning Officers ambao wanaopanga mipango ya shule.

Com. Lenaola: Go to the point, you don't go to the discussion.

John Mukal: Halafu pia, Teachers Employment should be done in the sub-locations to identify the few, so that it can assist those disadvantaged people in different districts because even also in colleges. Halafu kwa upande wa waalimu. Teachers are

very much under-paid. Teachers are getting very little salary, that is why you find that the teaching is not up-to-date. You find that the teacher is not engaged on business, because the salary which he earns is too little. He cannot maintain his family and other relatives which he supports. So teachers should get allowances like a Headteacher should at least get a responsibility of not less than 5,000/= because he is the manager of the school. The Deputy also is to get a reasonable amount and also teachers who are owning responsibilities in the school like game masters should have allowances.

Also transfer of teachers. Any teacher who will be transferred should be paid transfer allowance which is not less than 20,000/= because a teacher is moving from his station to somewhere on foot, while you find that the Government are being moved by lorries and other things to their stations. So a Headteacher should not again become a manager and at the same time the head of a class teaching, because now he is now serving a lot of masters – teaching and also doing the administration. He should only deal with administration only.

Now, discipline in schools: It has become a cumbersome at the moment when it has been ruled out that is what we call child rights. So the teachers are facing hard time and the children are becoming undisciplined. You find that children now burn one another in the dormitories because of lack of disciplines. So the disciplines should be within the school as usual. Any child who is found doing wrong should be given a recommended strokes by the school administration on the eyewitness by the parents. This is to reduce undiscipline in schools. So in case of any complaints that children die because of canes that one is a normal accident as usual.

Com. Lenaola: Last point mwalimu.

John Mukal: The last point is retirement age of a teacher should be 60 years. Because now when a teacher is about like me I am 45 years now and I am still very young and I am now gaining more experience in teaching and administration. So when a teacher is on 55 years he is now gaining more experience in schools.

Interjections: (Inaudible).

Ngalima Rutoronya: Mimi ni Ngalima Rutoronya. Mimi ni Councillor kutoka Putui.

Com. Lenaola: Councillor go straight to the point.

Ngalima Rutoronya: Sina mengi wale wandugu zangu wameongea yote pengine wamemaliza ile ningeongea. Zaidi ile ningeongea ni elimu. Kwa Katiba ya Kenya ningesema hivi, kwa elimu tuanzia nursery kwa Kenya nzima mpaka University iwe ya bure. Haya hiyo ni elimu na iwe sheria kwa kila mtu aweke mtoto kwa shule.

Haya utawala wa mkoa: Yaani kutoka PC mpaka DC mpaka DO mpaka Chief, Assistant Chief. Imekuwa ni shida sana kwa Katiba mtu anaambiwa tu wacha kazi bila kujitetea. Ningetaka watafute mtu yao moja ambayo wanachagua kumtetea ukweli wao.

Ya tatu, nasema tu kidogo kidogo sina mengi. Mambo ya mashamba. Sisi kama wa-Pokot ama Wakenya wengine wenye tulibaki nyuma sana kielimu ama vile serikali ilikuja mbeleni ile ya kwanza ya ukoloni walitunyanyasa kiasi fulani ambayo tukiangalia kama waPokot tuko na shamba yetu pale Trans-Nzoia ambaye tukiuliza ukweli wa mpaka tunaambiwa mpaka hamuna. Tukiangalia upande wa Turkana upande wa chini tunaambiwa hamna mpaka. Tungetake katika Katiba ya sasa serikali ya Kenya ituonyeshe mpaka zetu na kuchorea sisi mashamba yetu, ili tuwe na haki tusikosane na watu. Mimi nasema asante.

Com. Lenaola: Asantes sana Councillor. Joseph Lorian.

Joseph Lorian: Okay my names are Joseph Lorian. I am an Assistant Chief from Chepkope sub-location. My proposal or my opinion in this new Constitution is that, I would like education to be free for all from nursery to university. And again I would like the Local Government to be given that mandate to be under Central Government, because I am observing the Councillors are having a lot of problems. Yet a lot of money is being collected from the public, but some few are benefiting out of it.

And also I would like the Provincial Administration to continue. Most of our people have talked about it but they don't may be understand the good work the Provincial Administration is doing to keep law and order. If Provincial Administration will not be there, there will be a lot of insecurity. So I would like the Provincial Administration to continue the way it is and those who have education, to be considered to get higher salaries. Because we are being paid whether you are in university you get the same salary with somebody who don't have certificates. So we are seeing there, there is a lot of torturing for someone who has gone to school. So we would like somebody to be paid according to his education and also we would like those who will be in the field to get the Assistant Chief or the Chief to be form four and above.

And also, on Local Government those who vie for candidates should be form four and above, because in the croud we are getting right now somebody can be elected to be in the local government, but you can see somebody doesn't know his role. You can collide on the field with somebody is trying to do what you are supposed to do. And also we would like them to be trained those who will be qualified to show their role.

And also, I would like the new Constitution to consider her people to be given free piped water, because there was something I read in newspapers in 1987 when I was schooling secondary school. By the year 2000 everybody in Kenya will get piped water, right now it is 2002 we don't see good water, so I would like the new Constitution to consider to have people to get

piped water and also we are seeing you can now see some places in this area is hilly.

There is that land recommended for people to farm but you can see somebody farming over 45 degrees and a lot of erosion is being caused. The water catchment areas is disturbed, so we would like to get somebody from Provincial Administration let us say the area chief to be in charge of environment. Because we find in the current Constitution we have District Environment Officer but is somebody may he does not know the remote area like this place now where we are. So you can see people are entering in the preserved area for the forest people are tampering about it. So we would like the Chief to be given a full role to be in charge, although we have been given that chance, but some people somewhere the way my colleague has said somebody you can get false card saying that it should be done like this. So we would like the Chief to be given the Environment Officer and last I would like the new Constitution also to consider everybody or her citizens to get good roads. You can see now, I understand some of the Commissioners used air, but I wish you could use road so that you see the people of this country do not have good roads.

And also, what I would like to be put as law, especially in the Pokot we have lost so many ladies during labour days, because of FGM. It has caused a lot of lose to our ladies, so we would like in the new Constitution to be abolished. If you could ask the old men here you can see somebody has three wives, four wives. You know when the circumcised women have a problem when they have reached the age of 40 yrs they don't want to come close to the old man, because of that scar. So we are seeing there is a lot of problems, we would like that thing to stop because we are losing a lot of ladies during labour days. You can even ask here, during labour days many are operated.

For example, one time there was a lady whose husband was working in Nairobi then he went there during her labour day, went and asked the nurses who were ready to assist her so that it was not normal they called for the doctor to come for operation. That operation was not needed but because of that mark it brought a problem. So I would like that one to be stopped. That's all.

Com. Lenaola: Thank you very much. Please come and register there. Alexander Lemunyan? Benedict Loraita? Karibia hapo. Say your name and then go straight to the point.

Benedict Loraita: Majina ni Benedict Loraita ningependa kutoa pendekezo langu na la kwanza ni kuhusu elimu. Ninasema elimu iwe ya bure kutoka darasa la shule ya malezi hadi shule ya upili. Halafu university kama itakuwa expensive tuwe na cost-sharing na colleges. Pia, katika shule za malezi serikali iwaajiri wale waalimu katika Jamhuri yetu.

Ya pili, kuhusu sehemu hiyo ya elimu. Katika primary tuwe na specialization mahali ambapo tuna-monitor the progress of a child, towards class 8 to form 4 we gauge the of that particular child, ili tukipeleka katika chuo cha Technical Schools or may related issues so that by the year 2020 tuwe na wale ambao wanatoa utalamu katika nchi yetu.

Ya pili ni juu ya resources: Tumesema nchi yetu tuko na resources ya kutosha kabisa. Kwa hivyo hizi resources zitolewe kwa huduma ya wananchi wote.

Com. Lenaola: Proceed.

Benedict Loraita: Ya tatu, ni kuhusu land: Kama moja wapo wa resources. Ninasema land ownership kwa wakati huu iko katika trustland, iko katika registered land, iko katika community, communal ownership kwa hivyo tungependa kusema kwamba katika Katiba ijao tutoe all trustland, tutoe communal, halafu tuwe na registered land na issue of title deeds iwe available kwa mwananchi wote.

Halafu pia katika sehemu ile ya resources nilisahau kuna Commissioners of Land na Commissioner of Geology and Mines ambao wanahusika sana ku-bargain resources yetu wakiwa kule Nairobi na wanatoa title deed kwa mtu fulani kuchimba resources ambayo iko katika wilaya ya Pokot, bila kukuja kuuliza wenyeji. Kwa hivyo hawa watu jukumu hiyo wasipatiwe ila tu kwa ajili ya mwananchi mwenyewe ndio atakuja ku-bargain hiyo resource yake.

Kuhusu election, ninatoa maoni yangu hapa. Election ifanyike baada ya miaka tano vile na uchaguzi wa Madiwani na Wabunge ufanyike mwezi wa nane na uchaguzi wa Rais ufanyike mwezi wa kumi na mbili. Hapa katika uchaguzi wa Wabunge watakuwa wamepata Minister, Assistant Minister na makamu wa Rais. Halafu nitamaliza hiyo sehemu pia, hasa kwa wakati huu ambao tunaenda kusema uchaguzi usifanyike mwaka huu wengine wanasema mwaka ujao, na kwa maoni yangu ningesema ya kwamba uchaguzi ufanyike mwaka huu. Constitution isiwe linked na uchaguzi.

Kwa hivyo Constitution ni tofauti na election ni tofauti – those are different bodies. So tungependa pia Constitution iendeshe mambo yao hata kama tumewatengea pesa kwa wakati huu, iendeleo kufanya kazi yake na kufanya mawazo na baada ya hapo watuletee referendum hata wakati huu. Kwa sababu mmekuja kupata maoni ya watu. Kwa hivyo mtarudisha tena kwa sisi kwamba ile tumependekeza baada ya kufanya maoni ya Wakenya wote, hii ndio tulipata na mleta kwa wananchi ili tuangalie yale tulitoa kama siku ya leo ni vile ama hapana.

Kwa hivyo mambo ya kura iendeleo kama vile.

Com. Lenaola: Malizia.

Benedict Loraita: Halafu, pado kumaliza niko na tatu. Judiciary: Vile mtu alisema kwamba kortini hapa iwe kwa kila mtu. Kwa hivyo ningependekeza kwamba korti ambayo tutapatiwa upande huu wa mashambani ama nini, tuwe na mobile courts ambao wanahusika labda kwa wiki moja, mara mbili kwa wiki. Ili watu wakiwa pale wapeleke shida yao watatuliwe pale na

hivyo.

Upande wa tatu.

Com. Lenaola: Upande wa kumi.

Benedict Loraita: Kuna this capital death punishment. Death penalty – hatungependa kwamba kwa sababu human life is sacred and we are Kenyans who are religious. Kwa hivyo tungependa kwamba Kenya instead of death penalty tuwe na life sentence. Kwa wale ambao wamefanya shida kuu sana. Halafu.

Com. Lenaol: Second last point, we have not come to last.

Benedict Loraita: Okay, thank you. You are with me sure. Mambo ya katika Jamhuri yetu tuna jambo ambalo linaitwa Harambee. Na hii jambo ni muhimu kabisa katika Jamhuri yetu, lakini tukiangalia madhara yake nina kwa maoni yangu ninaona ni kubwa sana mambo ya harambee kama ni muhimu kwa Wakenya wale Wabunge wote wanatembea kutoka Nairobi mpaka Western na resources wanatumia, taxes ya wananchi. Ningependekeza kama kuna harambee iendelee tuwe na Ministry of Harambee & Funds – Wizara hiyo Fund Raising. Ambao watahusika ili pesa itengwe kwa ajili ya hiyo, kuliko kutuumiza kutumia magari kama mia moja na ni pesa ya wenyewe.

Com. Lenaola: Jambo la mwisho.

Benedict Loraita: Jambo la mwisho ni kuhusu religious sects. Katika Jamhuri yetu tunaona ya kwamba religious sects zinaanza ku-mushroom na tukiendelea katika hali hii mimi naanza yangu kesho, mwingine kesho kwa hivyo we shall have thousands and thousands. Na hii itaendelea mpaka kuwoko hata wakati huu tuko na ile devil worship. Kwa hivyo that one will erode them.

Com. Lenaola: Mwisho.

Benedict Loraita: Katika kura ijao kwa sehemu ya Chepnyal sehemu hii, eneo hili tuwe na constituency ambayo inaitwa Mtelo.

Interjections: (In Ki-Pokot dialect)

Com. Lenaola: Ngoja mzee tunataka heshima sana. Huu mzee ndiyo nimeita. Sema juna na kuendelea.

Loreng: *Kurenann Loreng.*

Com. Lenaola: Ngoja kwanza.

Loreng: *Mii tetanja nyoklentoy Turkwell nyo oketi yii tolapi kureriy piko walaka.*

Translator: Anasema kwamba tumenyonywa sana kama wa-Pokot. Kunyonywa kwetu ni kwamba tuko na nguvu za umeme hapa Turkwell ambayo haitufaidi kama wa-Pokot. Imetolewa na imeenda kufaidi mahali pengine.

Com. Lenaola: Basi pendekeza.

Loreng: *Pong'oo tetanyaa?*

Translator: Anasema kwamba haifai iende kwa kuwa ni yetu.

Com. Lenaola: Sawa sawa.

Loreng: *Ontee nyo koyar maat, kotu ani nyo opo ighsheo tagh.*

Translator: Anapendekeza kwamba kwa kuwa iko kwao ingekuwa ni mtu wa kwanza nguvu hii ya umeme iwafaidi, haingekuwa kwamba ifaidi mahali pengine.

Loreng: *Oyoran tetanyu akaghan ante!*

Translator: Anasema kwamba huyu ni ng'ombe wangu na anastahili kukamua.

Loreng: *Toh aswan loh mii choh nanto ewoh?*

Translator: Ili aone kwamba kuna maziwa ama hakuna.

Com. Lenaola: Basi hiyo tumesikia, jambo lingine.

Loreng: *Mokinoo kunet kle serikali monung' mpaka university.*

Translator: Anasema kwamba serikali ingeweza kutusomeshea wanafunzi kutoka darasa la kwanza mpaka university.

Loreng: *Akukonuu vitabunee ompo school.*

Translator: Pia serikali inafaa wapeane vitabu vya bure kwa wanafunzi.l

Com. Lenaola: Jambo linge mzee?

Loreng: *Kotonganjan loh toh kimi serikali nyaa?*

Translator: Basi ni mshangao kwamba anashangaa kwamba kuna serikali ama serikali tena haipo?

Com. Lenaola: Ungependekeza nini juu ya serikali?

Translator: *Yorenyi serikali kwich nee?*

Loreng: *Omoran serikali kuto monung' lowur masomo nko vitabun cho poh kleeh.*

Translator: Sasa yeye anapendekeza kwamba kuwe na elimu ya bure kwa wanafunzi wa primary na secondary na pia wapewe mahitaji yao kama vitabu na malezi na mengine.

Com. Lenaola: Hiyo tumesikia. Sema pendekezo lingine.

Loreng: *Omokan ketap kirwokot.*

Translator: Basi the issue of chiefs wapigwe kura.

Com. Lenaola: Jambo lingine?

Loreng: *Kegh nee serikali tomekirr monung'ee?*

Translator: Anaongea juu ya employment, kwamba watu wengi wako wamebaki tu. Ni kama kwamba serikali haina mpango wowote.

Com. Lenaola: Basi pendekeza?

Loreng: *Omokan serikali kwich ng'ala pichu motung' nyee kassu.*

Translator: Anataka serikali ijaribu kuwa na mpango kwa watu wake ambao wamesoma bila kuajiriwa.

Com. Lenaola: Kuja hapa na useme jambo moja tu. Jina lako? Umechukua kiti na nguvu. Sema jina kwanza.

Kemedar Cheptem: *Kurenann Kemedar wero Cheptem*

Translator: Anaitwa Kemedar Cheptem.

Kemedar Cheptem: *Korenyan nyai kong'alala pich nyai le Turkwell.*

Translator: Basi anasema kwamba watu wameongea saa zile zote na mimi ndiyo mwenyewe natoka huko Turkwell ndani.

Kemedar Cheptem: *Kikyonanun toketek bahari.*

Translator: Basi yeye ni mmoja wa wale ambao walifukuzwa kwa kutoka kwa hiyo bahari na alinyang'anywa sehemu yake.

Kemedar Cheptem: *Kiakaran, tok'mii serikali onto ewo?*

Translator: Sasa anasema ana njaa na ameshangaa kama serikali wako ama hawako?

Com. Lenaola: Pendekeza jambo.

Kemedar Cheptem: *Kekhuna maa bahari.*

Translator: Anasema sasa kwamba bahari imetoa moto.

Kemedar Cheptem: *Kowo rop korr anka.*

Translator: Pia kuongeza na kupoteza shamba pia moto ndiyo huo umetoka.

Com. Lenaola: Basi pendekeza mzee, pendekeza.

Kemedar Cheptem: *Omoran mat kropu aranu.*

Translator: Basi anataka kwamba moto huo ubadilishwe uje njia hii.

Com. Lenaola: Jambo lingine.

Kemedar Cheptem: *Mominye kirwokinto korenyan.*

Translator: Anasema kwamba sehemu hiyo hakuna chief.

Kemedar Cheptem: *Mominye tukul skul.*

Translator: Anasema kwamba sehemu hiyo hakuna shule.

Com. Lenaola: Basi pendekeza.

Kemedar Cheptem: *Omokan kekirr kirwokin aketek skul korenyan*

Translator: Anasema kwamba hasa anapenda serikali waandike chief kule na waweke shule.

Com. Lenaola: Pendekeza.

Kemedar Cheptem: *Momokanye kirwokot cho pkono kore anga*

Translator: Anasema kwamba watu wanatoka huku na wanakuja kuwa chiefs wa huko.

Kemedar Cheptem: *Amengut nyee shida koro nini!*

Translator: Sasa anasema watu wanatoka mbali na hawajui shida za huku.

Kemedar Cheptem: *Mutata tipun, michii nyo tung'eti korkenyi kuyou nyaa?*

Translator: Basi amekaa na mambo ya kutotairiwa kwa wasichana anataka wasichana watairiwe kwa kuwa hata wazazi wa hawa wasichana wametairiwa. Na hawo wangependa kubaki bila kutairiwa.

Kemedar Cheptem: *Tomutan tip'n.*

Translator: Anasema bado anatairi wasichana.

Com. Lenaola: Sawa. Jambo la mwisho.

Translator: *Nyo po sorom.*

Kemedar Cheptem: *Omoran kirwokin nko councillor kmi korenyan.*

Translator: Basi mwisho anarudia ile ya kwanza anataka Chief na Councillor wawe kule.

Kemedar Cheptem: *Akikuamanun tung'on nko rumbo. Omokan hospitali.*

Translator: Basi anaongea juu ya mbu na hospitali pia inatakikana kule isaidie wale watu ambao ni wagonjwa.

Kemedar Cheptem: *Omoran tukul paraparen kegh woni le korenyan.*

Translator: Barabara pia imekuwa ni shida, kwa kuwa watu wakipelekwa wanatumia machela kuleta watu upande huu. Anaongea juu ya barabara, barabara itengenezwe kuelekea kule.

Kemedar Cheptem: *Omoran serikali kwich korenyan kuten le koros walak.*

Translator: Sasa anataka serikali itengeneze maneno haya yote.

Com. Lenaola: Sawa sawa mzee. Asante.

Kemedar Cheptem: *Kwich koree kuten.*

Translator: Ili waweze kufanya sehemu hiyo ikuwe kama mahali pengine.

Com. Lenaola: Tumefika mwisho wa kikao na tungependa kuwashukuru sana watu wa Chepnyal kwa maoni yenu.

Translator: *Soroh nyoman pipo Chepnyal.*

Com. Lenaola: Kuna mtu alisema kwamba mngependa kuona haya maoni yakirudi tena muone kama tumeandika vizuri ama hatukuandika vizuri.

Translator: *Mii pich cho katep loh morecha kekirr tukuchaa nyo karam, ah yoku keswenacha.*

Com. Lenaola: Na baada ya kurudi Nairobi tutaandika unajua tumenasa kila mtu neno kwa neno.

Translator: *Kakikiracha ng'alechaye komwoy chi lowur.*

Com. Lenaola: Tutaandika hiyo report na kuwatumia kabla ya sisi kurudi hapa tena.

Translator: *Petechaa kekiroy ng'ale chona ake yonuchaa kurelu tomoh kepkancha napo.*

Com. Lenaola: Kwa hivyo mtaona kwamba Tukei amesema nini. Neno kwa neno.

Translator: *Osuwyekwaa loh ka mwane Tukei ndo chi anga tukul.*

Com. Lenaola: Na baada ya kuandika Katiba mpya tutawatumia hiyo Katiba muangalie kama ni sasa sawa ama si sawa sawa.

Translator: *Towonyo kikirata katiba, kuyonunechaa katibe toh asowuno atopchigh onto ewoo.*

Com. Lenaola: Kwa hivyo hii kazi ni yenu na lazima pia mkuwe involved kwa kila kiwango.

Translator: *Yighshonu nyingwaa nyu tolopai mokinoo omitekwa orii, ato k'petoy kepetoy tukul.*

Com. Lenaola: Na mimi kama binafsi ningependa kujua kama kuna mtu ako na barua yoyote kuhusu hii kanisa ya Roho, nijaribu kujua kama naweza kuwasaidia Nairobi.

Translator: *Pipo mafuta roho, ato mito palalianta, okonee towan ang'arakok ombo wol leh Nairobi.*

Com. Lenaola: Huyu ako na address yangu kama ningepata barua zenu nijaribu kuwasaidia pale mbele.

Translator: *Kakloh tung'etoGrace wono topoh tilyanu, tolopai atatungetekwa barua porwekwaa wolo opetutoh.*

Com. Lenaola: Ningependa kumuita mwalimu Mworio Aseme jambo moja halafu atuombee pia.

Translator: *Omoran kung'un yii mwalimu mworio kumwa kigh akong'a aksagh.*

Reuben Lomwai: Basi wana Tume na wananchi kwa jumla mimi ningetaka tu kutoa asante.

Translator: *Omoran oprchinee soroh pchu.*

Reuben Lomwai: Kwa hivyo sisi kama wakaaji wa Sok au Cheperiria Division tunafuraha nyingi sana leo

Translator: *Achoo yee le kasook ndo Chepareria division.*

Reuben Lomwai: Kujiunga na hawa wana Tume.

Translator: *Keghomo nko pipo tume.*

Reuben Lomwai: Kwa sababu wametuunganisha Jamhuri la Kenya nzima leo.

Translator: *Ombo wolo keghomityechaa nko Kenya .*

Reuben Lomwai: Siku hizi zingine tumekuwa tukisikia tu kwa redio hapa na pale.

Translator: *Taleh omotu kaklumechaa ompo redio.*

Reuben Lomwai: Lakini leo wako Chepnyal.

Translator: *Asete nyu achu mii Chepnyal.*

Reuben Lomwai: Kwa hivyo sisi tumefurahi sana na tumesisimuka kabisa.

Translator: *Kikng'orekchecha nyoman.*

Reuben Lomwai: Kwa hivyo nashukuru sana Alice Yano.

Translator: *Kle nyona nyo poh tagh oyokchinan soroh kamanu le Alice Yano.*

Reuben Lomwai: Pia huyu mwana Tume Isaack Lenaola.

Translator: *Klochichu leh Isaack Lenaola.*

Reuben Lomwai: Pia na waandishi wake au ma secretaries hawa Triza Apondi

Translator: *Nko pchono mii k'mwoghoy nyinde.*

Reuben Lomwai: Jomo Ngaithe.

Translator: *Nko nyona.*

Reuben Lomwai: Na pia Martina Odhiambo.

Translator: *Nko nyoni ng'at.*

Reuben Lomwai: Nyinyi mmekuwa marafiki zetu

Translator: *Kalukukwa kong'otyechaa.*

Reuben Lomwai: Na mmetuongoza vyema kabisa.

Translator: *Kopokwaa achaa ombo orr nyo kakchamachaa.*

Reuben Lomwai: Pia nashukuru ma-Councillors.

Translator: *Kakiyokchi soroh pchi le concillen.*

Reuben Lomwai: Hasa Councillor ya area hii Sok.

Translator: *Lenye Mukal nyu poh sook.*

Reuben Lomwai: Kwa vile ameandaa sisi vizuri na ametupokea.

Translator: *(In Ki-Pokot dialect)*

Reuben Lomwai: Pia tumeona Councillors

Translator: *Ombo wolo katak pich nyo karam.*

Reuben Lomwai: Tumeona hata wa Ptoyo.

Translator: *Nko chichu poh Ptoyo.*

Reuben Lomwai: Nyinyi tuko pamoja na nyinyi.

Translator: *Micha lowur nko akwaa.*

Reuben Lomwai: Na tunasema asante.

Translator: *Mwoghecha loh soroh.*

Reuben Lomwai: Tunashukuru vikundi mbali mbali ambao walijitokeza leo.

Translator: *Mito kruptino cho poh pich kiyokchinecha soroh tona kapkanaka yee.*

Reuben Lomwai: Kama Justice & Peace walikuwa hapa.

Translator: *Pipo Justice and Peace.*

Reuben Lomwai: Kanisa la AJC.

Translator: *Kanisanu poh AJC.*

Reuben Lomwai: Hata Mafuta Pole.

Translator: *Nko pchi poh Mafuta Pole.*

Reuben Lomwai: Na wale wengine wote mlishiriki kabisa.

Translator: *Nko akwaa lowurr.*

Reuben Lomwai: Nashukuru pia machiefs.

Translator: *Kloh akwaa kirwokot, soroh.*

Reuben Lomwai: Wa hapa Sok, Ptoyo, hata kule Chepkobe pia Chepereria huko tumeona wamefika mpaka pande hii.

Translator: *Krwokoti lowurr.*

Reuben Lomwai: Tunaona pia umuhimu ile tunapea kwa mambo ya Katiba.

Translator: *Kaswecha loh kaswekwa kighut nyopo katiba.*

Reuben Lomwai: Tunashukuru pia madam Grace.

Translator: *Madam Grace kakiyokunyi soroh.*

Reuben Lomwai: Licha ya ugumu ulioko katika kuandaa hii mambo ya Katiba.

Translator: *Kinnguto cha loh tkoh nyoman ng'ale chu poh kattiba.*

Reuben Lomwai: Tena yeye ni mdogo lakini umejaribu sana. Tunakushukuru na tunatakia wewe mazuri mbele.

Translator: *Atechinyi mining'. Yorchininyi ng'al cho karamach wono le tagh.*

Reuben Lomwai: Kwa hivyo kwa hayo machache ningesema tu sisi kama watu wa Sok tumefurahi sana kwa hawa maCommissioners.

Translator: *Leh pipo sook kaklecha soro.*

Reuben Lomwai: Tungojee na tutarajie kwamba Mungu atabariki mambo yetu na Katiba hii ijao italinda sisi na tutafurahia kama Jamhuri la Kenya.

Translator: *Kekanya yenyu pchu kpo kserr kasingwaa tokeh mburo le pipo Kenya.*

Reuben Lomwai: Labda tu kanjia moja ya kusema tumefurahia kwa kazi, hebu tupigie hawa makofi tatu tu halafu tuombe.

Translator: *Kerapaka nyu.Asoyon.*

Kesaghacha nyu.

Translator: Huyu atafunga kwa maombi.

Prayers: Basi natuombe, Baba katika jina la Yesu tunakushukuru kwa sababu ya siku ya leo. Asante kwa kazi ambayo

